

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TATU - TAREHE 2 NOVEMBA, 2006

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu baada ya kipindi cha maswali tutaingia katika zoezi la kuchagua miongoni mwa wagombea wa viti vile vya Bunge la Afrika Mashariki. Sasa namwagiza Katibu, Wagombea wote waje wakae *Speakers Galley* kwa sasa hivi na baadaye itakuwa rahisi kutoka hapo kuwapeleka kwenye chumba maalum ambacho kutokea huko ndiyo wataweza kuingia ukumbini kwa usaili.

Kwa hiyo, inatakiwa sasa wakae pamoja ili iwe rahisi kwa *Serjeant at Arms* baadaye kuwapeleka mahali maalum. Unajua jengo letu lilivyo. Itakuwa shida isije ikatokea mmoja wa wagombea hatukuweza kuhakiki yuko wapi akakosa haki ya kujieleza mbele ya Bunge hili. Kwa hiyo, Katibu ungesimamia hilo. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Na. 27

Ukubwa wa Majimbo Tanzania

MHE. ELIATTA N. SWITI (k.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI) aliuliza:-

Kwa kuwa, nchini Tanzania kwa sasa yamo jumla ya Majimbo 232.

(a) Je, kwa orodha ya Mikoa na Majimbo yake na ukubwa wa kila Jimbo (*sq. km*) yakoje?

(b) Je, kwa Majimbo ambayo ni makubwa kama Nkasi, je, Serikali inawasaidiaje Wabunge ili kazi yao isionekane kuwa ni adhabu ikilinganishwa na wenzao wenye Majimbo madogo?

(c) Je, ni nini tofauti ya kazi ya Mbunge, DC na DED katika kuleta maendeleo kwa wananchi, na zile fedha anazochangia Mkuu wa Mkoa na DC kwa wananchi ni za Serikali na kama ni hivyo, Mbunge naye atapewa lini kifungu kama hicho?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa hivi sasa yapo Majimbo ya Uchaguzi 232.

(a) Kutokana na uwingi wa majimbo hayo orodha ya Mikoa kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Majimbo ndani ya kila Mkoa na Wilaya na ukubwa wa kila Jimbo kwa *squire kilometre* ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali ambao amekabidhiwa Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nkasi ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 8,262 ambapo kiutawala ndilo Jimbo la Uchaguzi la Nkasi. Jimbo hili ni kubwa kwa eneo ukilinganisha na majimbo mengine yenye maeneo madogo. Hata hivyo, yapo Majimbo yenye maeneo makubwa kuliko Jimbo la Nkasi ambayo mengi pia ni Wilaya. Kwa uchache tu baadhi ya majimbo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Wilaya na Jimbo la Liwale lenye km. za mraba 33,031;

(ii) Wilaya na Jimbo la Sikonge lenye km. za mraba 24,335;

(iii) Wilaya na Jimbo la Simanjiro lenye km. za mraba 17,055;na

(iv) Wilaya na Jimbo la Tunduru lenye km. za mraba 17,694.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna Mbunge yeyote kutoka jimbo lenye eneo kubwa ambaye amepewa upendeleo wowote dhidi ya Mbunge anayetoka kwenye jimbo lenye eneo dogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa Majimbo ambayo yana maeneo makubwa ni kuyagawa kuwa Wilaya kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na uwezo wa Serikali kifedha. Utaratibu huu unarahisisha kazi ya utawala katika Mkoa husika na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya viongozi wa Kiserikali na Kisiasa katika maeneo husika.

(c) Mheshimiwa Spika, kazi za Mbunge ni pamoja na uhamasishaji wa maendeleo ya wananchi na uwakilishi wa wananchi Bungeni. Masharti ya kazi ya Mbunge kupitia Bunge yameelekezwa katika Ibara ya 63(2) kwamba Bunge litakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake

vyote katika utekelezaji wa majukumu yake na huo ndio uhusiano wa msingi kati ya Mbunge na kazi za Serikali.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 19 ya mwaka 1997 baadhi ya majukumu ya Mkuu wa Wilaya, ni pamoja na kuwa mwakilishi mkuu wa Serikali Kuu Wilayani, msimamizi wa Ulinzi na Usalama, Miongozo na Kanuni za Maendeleo. Jukumu la kusimamia miongozo na Kanuni za Maendeleo linaendana na majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji ambaye anayo majukumu ya kisheria na kiutawala katika Halmashauri na pia ni Katibu wa vikao vya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Mbunge, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wote wanatumikia umma na wanatekeleza majukumu yao kwa lengo la kuleta maendeleo ya wananchi. Tofauti waliyonayo ni utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia tofauti za masharti ya kazi na mgawanyo wa madaraka uliozingatia mihimili ya dola.

Mheshimiwa Spika, fedha anazochangia Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kwa wananchi ni za Serikali na malengo yake ni kusukuma nguvu na jitihada za wananchi katika miradi ya maendeleo na kujenga mshikamano kati ya Serikali na wananchi. Mbunge kama mwakilishi wa wananchi hushiriki katika uhamasishaji na kuchangia kadri hali inavyoruhusu. Serikali ipo kwenye mchakato wa kuangalia utaratibu unaofaa wa uwezekano wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, ili kuleta hali bora zaidi ya maisha kwa wananchi na hivyo kumshirikisha zaidi Mbunge katika kusimamia na kuratibu shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jimbo lake. *(Makofi)*

MHE. ELIATTA N. SWITI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Rukwa ni moja ya Mikoa mikubwa yenye Wilaya kubwa sana, je, upo uwezekano kwa Serikali kuona kwamba iko haja kwa Rukwa kuongeza Wilaya zake kwa mfano tukapata Wilaya ya Kalambo na Wilaya ya Katavi ili wananchi wa Rukwa waweze kupata huduma za Serikali kwa usahihi? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu, nilidhani nimemwona Waziri na ni mwenyeji wa Rukwa. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuomba kuanzisha Mikoa au Wilaya unaanzia kwenye Wilaya inayohusika na kupitia kwenye Mkoa unaohusika. Kwa bahati nzuri kwa hili suala ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Mbunge, tayari kikao cha Baraza la Ushauri cha Mkoa kilichokutana mara mwisho wali-table jambo hili kwa maana ya Wilaya, lakini wakaahirisha kidogo suala la Mkoa kwa kuwa linahitaji maelekezo kidogo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba angalau kwa sehemu ya pili ya sehemu ya swali lake tayari mapendekezo yamekwishawasilishwa yanasubiri kuletwa Serikalini. *(Makofi)*

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Njombe Magharibi liko Wilaya ya Njombe na ni kubwa kuliko majimbo mengine katika Wilaya ya Njombe, tuna majimbo matatu na sisi tuna vijiji zaidi ya 108 ambavyo ni nusu ya vijiji ambavyo vipo katika Wilaya ya Njombe na kwa kuwa Waziri Mkuu alipokuja alisema kwamba kuna uwezekano kwamba ningepomba Wilaya katika Njombe Magharibi naweza nikapewa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kunipatia Wilaya ili walau na sisi tuwe na maendeleo ya kutosha kwa sababu tuko pembezoni mwa Wilaya yetu na tuna tatizo kubwa tulipokuwa tunaomba Mkoa ilishindikana lakini Wilaya tuliambiwa tunaweza tukapewa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa, tena rafiki yangu Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwanza una bahati kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alikupa hiyo nafasi ya kukupa matumaini ya kupata Wilaya. Lakini pamoja na hilo bado nitaomba jambo hili mliwasilishe kwanza katika Wilaya yenu kupitia Halmashauri yenu, kisha iende mpaka kikao cha *RCC*, baadaye sasa ije kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa maana ya kuona kama taratibu na misingi ipo ya kuweza kukupa Wilaya katika Jimbo hilo. (*Makofi*)

Lakini niseme vile vile kwamba kwa bahati mbaya mlikuwa mmeomba Mkoa wa Iringa, nao ugawanywe katika Mikoa miwili mkitaka Njombe iwe Mkoa. Nadhani majibu mliyapata kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ile alipokuwa huko. Kwa hiyo, nadhani hili msisumbuke sana nadhani muendeleo na juhudi za Wilaya. (*Makofi*)

Na. 28

Kupanda Hadhi Mji Wa Sanya Juu

MHE. MICHAEL L. LAIZER (k.n.y. MHE. AGGREY D. J. MWANRI) aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Sanya Juu unaendelea kukua kwa haraka; na kwa kuwa kivutio kikubwa cha shughuli za biashara na unaunganishwa na maeneo mengine muhimu kama mashamba makubwa yaliyopo *West Kilimanjaro* ya *NAFCO* na *NARCO* na vile vile minada mikubwa.

Je, kwa nini Mji huo usipandishwe hadhi na kuwa Mji Mdogo ili kuharakisha na kusukuma maendeleo ya wananchi waishio katika eneo hilo na wale waliopo jirani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kijiji kiweze kupewa hadhi ya kuwa Mji Mdogo, kinatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

(i) Kuwa na wakazi wasiopungua 10,000;

(ii) Kuwa na huduma muhimu kama vile za afya, soko, maduka yasiyopungua 20 yenye leseni, Mahakama ya Mwanzo na shule ya sekondari;

(iii) Pia kijiji kiwe Makao Makuu ya Kata au Tarafa; na

(iv) Kijiji kiweze kujiendesha kimapato.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaofuatwa kufanya kijiji kuwa Mji Mdogo ni pamoja na:-

(i) Kijiji husika kupeleka maombi katika ngazi ya Halmashauri.

(ii) Halmashauri kujadili ombi kwa kuzingatia vigezo ili kuona kama kijiji kinakidhi vigezo hivyo.

(iii) Endapo kijiji kina sifa, kijiji na Halmashauri itaandaa maelezo ya mipaka na ramani.

(iv) Halmashauri na Kijiji ibuni nembo ya kutambulisha Mji unaokusudiwa.

(v) Baada ya kukamilika taratibu zote zitawasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye atatangaza Mji huo kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili Kijiji cha Sanya Juu, kipandishwe hadhi ya kuwa Mji Mdogo, nashauri Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji cha Sanya Juu kuangalia kama kinakidhi vigezo nilivyovitaja hapo juu. Vile vile wafuate utaratibu ulioelezwa wa kutuma maombi katika ngazi husika.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri aliyotoa na mimi nafahamu Mji wa Sanya Juu kwa sababu tunapakana na Tarafa yangu ya Endui ambayo inapata huduma hapo Sanya Juu na kwa kuwa vigezo vyote alivyotaja Naibu Waziri vyote vimekamilika, ni vitu viwili tu ndiyo bado havijakamilika ambavyo ni pamoja na nembo.

(a) Je, watakapokamilisha nembo pamoja na kuleta maombi mtawakubalia?

(b) Kwa kuwa kuna mashamba mengi yanayozunguka Mji wa Sanya Juu kama alivyoeleza Mbunge kwenye swali la msingi na kwa kuwa Mji wa Sanya Juu hawana

maeneo, je, Serikali iko tayari kuwasaidia kuwapa hayo mashamba yaliyozunguka Mji huo ili Mji huo uweze ukapanuka?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali la pili halihusiki, suala la kugawa mashamba ili iwe eneo ni tofauti na swali la msingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri utajibu swali la kwanza la nyongeza.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba iwapo vigezo vinavyohusika vitatimizwa, Serikali iko tayari kutoa kibali cha kijiji hicho kuwa Mji Mdogo. Lakini pamoja na hayo pia inategemeana na hali ya kifedha ya Serikali.

Na. 29

Hati za Kumiliki Viwanja vya Makazi

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu ramani ya viwanja vya Mji wa Ludewa, zikamilike na kuwasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi bila marejesho na hivyo kuendelea kuwanyima wananchi hati ya kumiliki viwanja hivyo na kujenga mji wao:-

Je, ni lini Kamishna wa Ardhi ataridhia ramani hizo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo:-

Kwanza si kweli kuwa Wizara haijarejesha ramani za viwanja vya Mji wa Ludewa kwa muda mrefu. Aidha, Kamishina wa Ardhi hausiki na kuridhia michoro ya viwanja.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1990 Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa iliwasilisha Wizarani kwangu ramani tisa kwa ajili ya kuhakikiwa, kuidhinishwa na kisha kusajiliwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ramani zote tisa zenye jumla ya viwanja 392 zimekwishasajiliwa na kutumwa kwenye Halmashauri husika kwa ajili kuwezesha umilikishaji wa viwanja kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ramani hizo zilianza kutolewa kwa Wilaya ya Ludewa tangu mwaka 1991 kama ifuatavyo, mwaka 1991 ramani mbili zenye viwanja 74, mwaka 1999 ramani moja yenye viwanja 10, mwaka 2000 ramani moja yenye viwanja 118, mwaka 2001 ramani mbili zenye viwanja 124, mwaka 2002 ramani moja yenye viwanja 58,

mwaka 2003 ramani moja yenye viwanja sita na mwaka 2006 ramani moja yenye viwanja viwili.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna ramani yoyote ya kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ambayo haijaidhinishwa. Hivyo, napenda kuihimiza Halmashauri ya Ludewa kupitia Kamati yake ya kugawa ardhi kuharakisha umilikishaji wa viwanja hivyo kwa wananchi ili wapate hati na kuijenga mji wao.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba miji midogo kama vile Nyaguge, Kabila ambayo siyo makao makuu ya Wilaya lakini inakuwa haraka, ina mpango wa kuwezesha maeneo hayo na vijiji hivyo vikubwa kupimwa ili vikue kwa mpangilio badala ya kuachia wananchi wajenge holela. Kwa nini Serikali isiruhusu Serikali za vijiji zipime zenyewe zipange maeneo hayo badala ya kuachia wananchi wajenge holela?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba Miji midogo, Miji mikubwa na Majiji yanapimwa kwa kiwango kikubwa kuanzia mwaka 2000/2001. Kuna Mfuko wa Kupima Viwanja ambao unaitwa *Plot Development Revolving Fund* ambao kwa sasa una milioni 417 na fedha hizo zinakopeshwa katika Halmashauri mbalimbali ili kuwezesha kupima viwanja. Ningeomba Waheshimiwa Wabunge wawasiliane na Halmashauri zao ili kuhimiza waweze kuleta michanganuo katika Wizara yetu tuweze kuwakopesha hizo fedha kuhakikisha kwamba viwanja vinapimwa.

Pili, ameuliza kwa nini hatuwezi kuwaruhusu Halmashauri za Vijiji viweze kupima viwanja kupunguza ujenzi holela. Ngingependa kujibu kwamba vifaa vya kupima viwanja ni gharama kubwa. *GPS* ndiyo inatumika kwa teknolojia ya kisasa kupima viwanja ambapo *GPS* moja ni milioni 32 na Halmashauri hazina uwezo wa kuzinunua. Kwa hiyo, kwa sasa bado tunazidi kuwasaidia kutoka Serikali Kuu ambao tunatumia *GPS* na wale ambao *theodolite* za zamani zinafanyakazi bado tunawaruhusu kupima viwanja. (*Makofi*)

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ndiyo iliyohusika katika kuchora mipaka kwa kuzingatia koo pale Tarime na hatimaye kutozingatia kwamba hii hii ardhi ingepungua, je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha ile mipaka na vile vile kuwapa ardhi zaidi watu wa Tarime ili wasiendelee kuuana?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kidogo nilikuwa naliona kama liko nje kidogo lakini kwa kuwa una maelezo.

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mipaka ya vijiji ya Wilaya na Mikoa tumekwisha waandikia Wakuu wa Mikoa wote katika nchi nzima ili *Government Notice* ambazo zimetolewa za kupanga maeneo katika maeneo katika Mikoa na Wilaya husika ziweze kutumika ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Mkoa kwa Mara kwa hiyo, nina uhakika kwa kupitia hiyo *Government Notice* ambazo zimetolewa ambazo zimeanzisha hizo Halmashauri zitamsaidia Mheshimiwa Chacha Wangwe kujua maeneo ya mipaka yanayohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini napenda pia kuahidi kwa Mheshimiwa Chacha Wangwe, naweza nikampa nakala ya *Government Notice* ya Mkoa wa Mara ambayo inaweza ikamsaidia kutambua mipaka na maeneo ya sehemu zinazohusika tukiwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Na. 30

Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kutowatesa Mahabusu na Wafungwa

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu mpaka sasa haijaridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kutowatesa Mahabusu na Wafungwa na kwa kuwa katika Bunge la mwaka 2000 - 2005, Bunge la Bajeti 2004 niliuliza suala hili na Serikali ilijibu kuwa itaridhia katika Bunge la Februari 2005 lakini mpaka sasa swali hili linaulizwa mkataba huo haujaridhiwa.

Je, kuna sababu gani za msingi zilizosababisha kutoridhia mkataba huo?

SPIKA: Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Naibu Waziri huyu ni mgeni katika Wizara hiyo. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakiri kwamba swali hili liliulizwa katika Bunge la Bajeti 2004, kama alivyosema Mheshimiwa Shoka Khamis Juma. Hata hivyo si kweli kwamba Wizara yangu iliahidi kuuleta mkataba huo katika Bunge la Februari 2005, bali Waziri iliahidi kuuleta mkataba huo baada ya muda si mrefu, pengine mapema 2005, kwa kutegemea kwamba taratibu zote zingekuwa zimekamilika.

Kwa kuzingatia hilo, Wizara ya Katiba na Sheria zimekwishachukua hatua za awali za kushughulikia uridhiaji wa mkataba huo unaojulikana kama *The Convention Against Torture and other Cruel Inhuman or Degrading Treatment or Punishment* kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo ni pamoja na kuandaa rasimu ambayo kwanza itapelekwa kwa wadau ili ijadiliwe tupate maoni ya wadau na baadaye iwasilishwe Serikalini kwa maamuzi.

Baada ya hatua hizo muhimu kukamilika mkataba huo utaletwa katika Bunge hli ili kama litaridhika liuridhie mkataba huo. Ushirikishwaji wa wadau wote wanaohusika na maudhui yaliyomo katika mkataba huo, ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, asasi za Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na kadhalika ni jambo la msingi linalopaswa kufanywa kabla ya kuuleta Mkataba huo hapa Bungeni ili uridhie.

Aidha, tulihitaji muda wa kutosha wa kupitia Sheria zinazohusika ili kujiridhia kwamba hazipingani na masharti ya mkataba huo na kujiridhishe kwamba ni kwa maslahi ya nchi, kama tutauridhia Mkataba huo. Mkataba huu hauwahusu mahabusu na wafungwa tu ila mambo mengine yanayohusu sera kama vile matumizi ya adhabu ya viboko mashuleni, matumizi ya viboko kama adhabu inayotolewa na mahakama, utoaji wa adhabu ya kifo kwa makosa ya mauaji ya kukusudia na uhaini na utoaji wa adhabu kwa makosa ya jinai.

Mheshimiwa Spika, wakati ukifika Waheshimiwa Wabunge, watahusishwa kikamilifu katika uridhiaji wa Mkataba huu na bila shaka kabla ya hapo Waheshimiwa Wabunge, watahiriki katika majadiliano yatakayofanywa kupata maoni ya wadau. Kama Wizara yangu ilivyosema wakati wa kujibu swali Na. 3617 alilouliza Mheshimiwa Mbunge, wakati huo, nchi yetu ingawa haijaridhia Mkataba huo, inatekeleza maudhui yake ambayo yamo pia katika Katiba ya nchi yetu.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, Serikali ya Awamu ya Nne imepanga katika Mkutano wa ngapi kuridhia Mkataba huu? Swali la kwanza.

Swali la pili, kwa kuwa Serikali iliahidi hapa Bungeni kuwa itaridhia Mkataba huu mwezi Februari 2005 na haikufanya hivyo, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kuwa Serikali inapotoa ahadi hapa Bungeni ya kufanya kitu na badala yake isifanye inalipotosha Bunge pamoja na wananchi wanaotusikiliza? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema katika jibu letu la msingi nia ya Serikali ilikuwa kuuleta Mkataba huo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuuridhia. Lakini kama nilivyoeleza, kuna taratibu ambazo zinatakiwa kufuatwa na ndiyo Serikali sasa hivi iko katika harakati na mchakato kuhakikisha kwamba taratibu zote zinafuatwa kikamilifu ili iletwe mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya uridhiaji. (*Makofi*)

Naomba nirudie kwa kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Nne pamoja na Serikali ya Awamu ya Tatu haijawa na mpango wa kudanganya wananchi na tunahakikisha kwamba taratibu za kisheria zinafuatwa kikamilifu muda wote. (*Makofi*)

Tatizo la Umeme Nchini

MHE. BENSON M. MPESYA aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na tatizo la uhaba wa umeme na sababu kubwa ikiwa ni upungufu wa maji katika Bwawa la Mtera.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizobainishwa kwa chanzo cha upungufu huo mkubwa wa maji?

(b) Je, ni baada ya muda gani Bwawa hilo linatarajiwa kuwa na maji ya kutosha?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lakini kabla sijafanya hivyo naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bwawa la Mtera ni bwawa kubwa nchini linalotumika kuhifadhi maji kwa ajili ya kuendesha mashine za uzalishaji umeme wa Mtera zenye uwezo wa kuzalisha jumla ya *MW 80*. Baada ya hapo maji hayo huendelea hadi Kidatu ambako hutumika kuzalisha umeme kwenye mashine zenye uwezo wa kuzalisha jumla ya *MW 200*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu za msingi zilizobainishwa kuwa chanzo cha upungufu mkubwa wa maji ni kama ifuatavyo:-

- Ukosefu wa mvua kwenye vyanzo mbalimbali vya maji ya mito inayotiririka kwenye Bwawa la Mtera.

- Ongezeko la matumizi ya maji kwa shughuli za kilimo katika maeneo ya mabonde ya Usangu, Kapunga, Pawaga na maeneo ya Mtera.

- Ongezeko la matumizi makubwa ya maji katika kuzalisha umeme kuliko matumizi ya gesi na mafuta, jambo ambalo Serikali inalichukulia hatua.

(b) Mheshimiwa Spika, Bwawa la Mtera linatarajiwa kuwa na maji ya kutosha iwapo zitanyesha mvua za kutosha katika msimu ujao wa mvua pamoja na kuwapo kwa udhibiti wa matumizi ya maji, *TANESCO*, wakulima na wafugaji, katika maeneo yaliyotajwa.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili madogo ya kuuliza. Swali la kwanza, je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja ya kupeleka wataalam wa kwenda kuchunguza hasa hasa matatizo yanayolikabili bwawa la Mtera kwa uhaba wa maji. Kwa sababu baadhi ya tafiti zimeonyesha kwamba kulikuwa na *unnecessary drawing of water below minimum level?* Naliomba hilo lifanyike.

Swali la pili, kwa kuwa Serikali iliahidi hapa Bungeni kwamba itasambaza umeme katika vijiji vya Mbeya, je, Serikali itakuwa tayari kabla ya kufanya hivyo kupeleka vifaa vya *service line* ambavyo vimekuwa ni haba kwa *TANESCO* Mbeya ili usambazaji uwe rahisi zaidi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la pili halihusiani kabisa na swali la kwanza. Kwa sababu swali hili lilikuwa linauliza juu ya uwezo wa Mtera sasa anazungumzia tena kutawanya nguzo. Lakini kama unadhani unapenda tu kuliarifu Bunge pia vizuri tu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli kwamba bwawa la Mtera kwa mara ya kwanza tangu lijengwe mwaka 1981 limepatwa na matatizo ya uhaba mkubwa wa mvua na maji ya pale. Ni kweli pia kwamba wataalam mbalimbali wameishauri Serikali kwamba ipo haja ya kufanya tathmini ya kina ya kuelewa kwa nini maji yanapungua hata wakati wa mvua inapokuwa kubwa. Ningependa kumshauri na ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali italiangalia suala hilo na kuona uwezekano wa wataalam kufanya tathmini ya kina na kuishauri Serikali.

Kuhusu suala la Mbeya Vijijini kupatiwa umeme, tulilijibu swali hili siku mbili zilizopita. Lakini ningependa tena kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali katika mpango wake wa *Rural Electrification* umeipa Mbeya kipaumbele na katika pesa zilizopatikana shilingi bilioni 10.55 Mbeya iko katika kipaumbele kwa maana hasa ya kupanua *transformers* za Mbeya lakini pia kununua vifaa mbalimbali vya Vijiji vya Mbeya ili kuhakikisha kwamba wanapata umeme wa *thermo* yaani wa mafuta wakati tukisubiri mvua za Mtera zinyeshe.

Na. 32

Mradi wa Umeme wa *Grid*

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kuwa utapatiwa umeme wa gridi wa *132 KV* kutoka Makambako hadi Songea na kwa kuwa ufuatiliaji wa mradi huu umeonyesha ya kuwa kazi ya kufanikisha ujenzi wa laini hiyo ulikuwepo ni katika hatua za awali za kupasisha mradi na kwa kuwa wananchi wa Ruvuma wanafuatilia mradi huo hatua kwa hatua:-

(a) Je, ni ratiba ipi ya utekelezaji wa mradi huo Serikali itawapa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma ili na wao waweze kwenda sambamba na mradi huo?

(b) Je, mradi huo utagharimu jumla ya shilingi ngapi za Kitanzania au dola za Kimarekani?

(c) Je, fedha hizo zinagharimiwa na nani na zimeshatolewa au mipango ikoje?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge Viti Maalum, lakini kabla sijafanya hivyo naomba pia kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO*, inayo mikakati ya kupeleka umeme wa gridi kwenye mikoa ambayo haijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Mkoa wa Ruvuma kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne ni mmoja kati ya mikoa itakayounganishwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa kutoka kwenye kituo cha kupozea umeme cha Makambako kinachoendelea kujengwa chini ya ufadhili wa Serikali ya Sweden. Umeme huo utakuwa wa kilovolti 132 na ukifika Songea utapozwa ili kutumika Songea na kusambazwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya za Mbinga na Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ratiba ya utekelezaji wa mradi huo ni kama ifuatavyo:-

· Taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu imefanywa na imeshawasilishwa *SIDA* - Sweden ambayo inafadhili upembuzi huu. Taarifa hiyo, ilikamilika na kuwasilishwa kwa mfadhili mwezi Februari, 2006.

· Baada ya fedha za utekelezaji kupatikana, hatua itakayofuata itakuwa kumchagua mshauri wa mradi ambaye atatayarisha zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mradi ikiwa ni pamoja na kujenga njia za umeme wa kilovolti 132 kuanzia Makambako hadi Songea pamoja na laini ya kilovolti 33 kwenda Makao Makuu ya Wilaya za Mbinga, Ludewa na Namtumbo.

(b) Gharama za mradi huu hadi kukamilika zinakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 43.5.

(c) Mheshimiwa Spika, fedha hizo zitagharimiwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la *SIDA*. Aidha, fedha za hapa nchini zitakazotumika katika utekelezaji wa mradi huu ni shilingi bilioni mbili.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne ya Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza ahadi zake. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa ni kwamba umeme unaotoka Makambako mpaka Songea wa gridi na kuelekea Namtumbo ambao utapitia vijiji kwa mfano Madaba, Wino na kwenda Namtumbo kuna vijiji kama Suluti, Hanga, Namabengo, Namkongo na kwenda Mbinga kuna Peramiho, Likonde, Kigonsera, mpaka Mbinga. Sasa tayari sisi wananchi wa kule tumeshakuwa na mpango wa kuhakikisha kwamba nyumba zote zinaezuliwa nyasi na kuwekwa bati ili tuweze kupata umeme huo. (*Makofi*)

Lakini pamoja na mpango huo tunaomba pia kufahamu Serikali ina mikakati ipi ya kuwawezesha wananchi hao kupata maendeleo zaidi kutokana na umeme huo? (*Makofi*)

Swali langu la pili, naomba pia kukuomba Mheshimiwa Waziri, kwamba mara ya mwisho wananchi kutoka maeneo ya Magagula na Lusonga hasa wale wa Taasisi ya JKT pale Mlale walikuwa wameomba waunganishwe kwenye umeme wa Chipole ambao ulionekana ni mdogo kwa kuwa una Kilowati 400 tu. Lakini katika huu umeme wa gridi kwa kuwa kuna *line 33 KV* itakayoenda mpaka Mbinga na kutoka Mbinga kwenda Mlale ni umbali usiyozidi kilometa 30. Kwa hiyo kama itaenda *line* ya *KV 33*...

SPIKA: Swali Mheshimiwa!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Ndiyo naendelea Mheshimiwa. Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuanza kufanya tathmini ya kutoka Mbinga na kuwapelekea JKT Mlale pamoja na wananchi wengine? Ahsante sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri natumaini majibu yako hayatakuwa marefu kama maswali yaliyoulizwa. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, yatakuwa mafupi zaidi kuliko maswali.

Moja, kuhusu suala la vijiji vinavyotoka kuanzia Makambako, Songea hadi Mbinga Serikali sambamba na kupeleka gridi hiyo Songea hadi Mbinga, imepanga pia kupeleka *transformers* au vituo vya kupoozea umeme katika vijiji vyote kuanzia Makambako, Songea hadi Mbinga ili kuwawezesha wananchi wa maeneo ya Madaba, maeneo ya Wino, maeneo ya Songea Vijijini kufaidika na umeme huu kwa maendeleo yao. (*Makofi*)

Pili, kuhusu suala la umeme *KV 33* kutoka Mbinga hadi JKT Mlale ambao unaonekana hautoshi, Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa sababu Mbinga kama nilivyosema siku mbili zilizopita imepangiwa shilingi milioni 500 za kwanza za awali kwa ajili ya umeme na tunadhani baada ya kuweka *transformers* hizo watu wa JKT Mlale wataweza kupata umeme na vijiji vya karibu kama tulivyoahidi. (*Makofi*)

Uhamaji wa Kituo cha Polisi - Kalinzi

MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-

Kwa kuwa Kalinzi ni moja kati ya vijiji ambavyo Serikali imevitangaza kuwa miji midogo; na kwa kuwa kijiji hicho chenye wakulima wa Kahawa kimekuwa na sasa kina watu wengi, lakini hakuna kituo cha polisi kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa raia na mali zao:-

Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha polisi Kalinzi?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kijiji cha Kalinzi kinahitaji kuwa na kituo cha polisi, lakini kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kwa sasa hakuna mpango wa kujenga kituo hicho katika eneo hilo. Hata hivyo kwa wakati huu kijiji kitaendelea kupata huduma ya polisi kutoka vituo vya Manyovu, Mahembe na Mwandiga. (*Makofi*)

Aidha, kutokana na maombi mengi ya Waheshimiwa Wabunge juu ya mahitaji ya vituo vya polisi katika maeneo mbalimbali nchini, Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi inaandaa mpango maalum (*master plan*) ili kujua mahitaji halisi ya vituo vya polisi nchini kufuatana na vigezo vinavyokubalika kipolisi na mazingira ya sasa na baada ya kukamilika kwa mpango huo utawasilishwa Serikalini ili kuondoa tatizo hili kwa muda mrefu ujao.

MHE. MANJU S. O. MSAMBYA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza na nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Naibu Waziri anaposema kwamba kijiji hiki kitapata msaada wa polisi kutoka Manyovu na Mwandiga, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba hali ya usafiri kutoka Manyovu kuja Kalinzi na kutoka Mwandiga kwenda Kalinzi siyo nzuri kiasi kwamba likitokea tukio lolote lile polisi watashindwa kufika kwa wakati na hivyo kilanachokusudiwa kufanywa na polisi kitakuwa hakiwezi kupatikana?

SPIKA: Hili swali linahusu matengenezo ya barabara. Kwa hiyo, siwezi kuliruhusu liulizwe kwenye Usalama wa Rais, tunaendelea.

Niseme tu kitu kimoja, leo kimenishangaza ni kwa nadra sana Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, aulize swali la msingi halafu asiulize la nyongeza. Lakini ndiyo maendeleo hayo. (*Makofi*)

Na. 34

Tatizo la Ujambazi wa Kutumia Silaha Ngara

MHE. PROF. FEETHAN F. BANYIKWA aliuliza:-

Kwa kuwa kuna matatizo makubwa ya ujambazi wa kutumia silaha katika Wilaya ya Ngara hasa Tarafa za Murusagamba na Rulenge:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa wananchi wa Tarafa hizo, hasa vijiji vya Kesa, Kabaheshi na Mulonzi wanaishi kwa amani bila hofu ya kuvamiwa na majambazi ya mara kwa mara?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Feethan Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua matatizo makubwa ya ujambazi katika Wilaya ya Ngara na vijiji mbalimbali vikiwemo vya Kesa, Kabaheshi na Mulonzi katika Tarafa ya Murusagamba na Rulenge. Ili kukabiliana na hali hii Serikali kupitia vyombo vya Ulinzi na Usalama inaendesha operesheni maalum za mara kwa mara kusaka majambazi, wahamiaji haramu na wanaomiliki silaha kinyume cha Sheria. Operesheni hizi zinafanyika nchi nzima hasa mikoa ya mipakani yakiwemo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Pia wananchi wa Tarafa ya Murusagamba na Rulenge na hasa vijiji vya Kesa, Kabaheshi na Mulonzi wameshirikishwa katika masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo yao kwa utaratibu wa Polisi Jamii.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kuwashirikisha wananchi na mapambano dhidi ya vitendo vya ujambazi na uhalifu mwingine, yamefanyika kwa mafanikio makubwa ambapo Mkoa wa Kagera peke yake jumla ya silaha haramu 240 zimekamatwa au kusalimishwa pamoja wahalifu mbalimbali kutiwa mbaroni.

Aidha, jitihada hizi zitaendelezwa ili kumaliza uhalifu katika maeneo husika na maeneo mengine nchini kwa nia ya kuwaondolea hofu wananchi wetu ili waweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, bado kuna baadhi ya wananchi wachache wanaoshirikiana na wahalifu na kuficha kutoa siri na kuficha kutoa taarifa kwa polisi, naomba kutanabahisha kuwa vita dhidi ya uhalifu vinahitaji ushirikiano wa dhati

baina ya wananchi na Jeshi la Polisi, naomba tushirikiane tukomeshe uhalifu nchini kwani kila Mtanzania ana wajibu wa kuilinda Tanzania. *(Makofi)*

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyejibu swali kwa ukamilifu na kwa maana hiyo ninaomba niulize swali kwa ukamilifu na kwa maana hiyo ninaomba niulize swali la nyongeza. Je, kwa kazi nzuri hiyo anayoifanya ataahidi ya kwamba kwa sababu wavuvi wa Wilaya ya Ukerewe na Muleba, Sengerema, Mara wanasumbuliwa sana na majambazi na kuibiwa vifaa vyao vya uvuvi atushirikishe sisi Wabunge wa huko ili tuweze kufanya kazi na atuletee hiyo usafishaji maalum ndani ya maji ili wavuvi waendeleo kufanya kazi yao kwa amani? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote ili kuhakikisha tunapambana na majambazi katika maeneo ya Ziwa Victoria na kwingine kokote nchini. Kwa sababu kuanzishwa kwa utaratibu wa Polisi Jamii nia kubwa ni kuwashirikisha wananchi wote ili tupambane kuondoa uhalifu huo.

Kwa wakati huu operesheni maalum imeanzishwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kupambana na ujambazi nchini na mafanikio makubwa yamejitokeza.

Na. 35

Umaskini Uliokithiri kwa Wanawake

MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. MARTHA J. UMBULLA) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imeahidi kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa madhumuni ya kupunguza umaskini nchini chini ya mkakati wa MKUKUTA; na kwa kuwa umaskini uliokithiri unapimwa kwa vigezo mbalimbali:-

(a) Je, Serikali itatumia vigezo gani kupima umaskini uliokithiri na hivyo kuyapa kipaumbele maeneo ya kuanzia?

(b) Je, Serikali inaelewa kuwa Mkoa wa Manyara una makabila yaliyo maskini sana kwa mfano, Hadzabe na hivyo kustahili kuanza na jamii hizo?

NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inapima umaskini uliokithiri katika ngazi ya kaya kwa kupitia viashiria mbalimbali ikiwa ni pamoja na idadi ya milo kwa siku, aina na ubora wa makazi, madhara ya lishe - utapiamlo, kiwango cha kudumaa na kusinyaa, wastani wa pato la kaya kwa mwaka, kiwango cha elimu cha mkuu wa kaya, upatikanaji wa maji safi na salama, idadi ya wategemezi katika kaya na fursa za utumiaji na umiliki wa rasilimali.

Aidha, vigezo mbalimbali kama vilivyoainishwa hapo juu vinapimwa kupitia tafiti, kama vile tafiti ya hali ya matumizi ya kaya (*Household Budget Survey*), tafiti ya hali ya ajira (*Labour Force Survey*) na Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi (*National Poverty and Housing Census*).

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali inatambua kuwa Mkoa wa Manyara una makabila yaliyo nyuma kimaendeleo likiwemo kabila la Hadzabe. Serikali ilishafanya tafiti za hali ya umaskini na maendeleo na kubaini kuwa uathirikaji wa umaskini unatofautiana kiwilaya. Wilaya nyingine zimeathirika zaidi katika baadhi ya viashiria ikiwemo Wilaya ya Mbulu na Iramba walipo kabila la Hadzabe. Serikali kwa kupitia programu mbalimbali zikiwemo programu za kuondoa umaskini zinazoendeshwa na Halmashauri, Mkoa, Wilaya, Wizara mbalimbali na *TASAF* pamoja na mpango wa uwezesaji wa wananchi wa zile bilioni moja kwa kila mkoa zote hizi zimelenga katika kuboresha maisha ya Watanzania wote kwa ujumla na hasa katika maeneo ambayo yenye umaskini uliokithiri. (*Makofi*)

Aidha, Serikali itaendelea kushawishi asasi za kijamii na wahisani mbalimbali kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuongeza nguvu zao katika miradi ya kiuchumi, kijamii katika jamii zilizo nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wafuatao, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge wa Mbulu na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kwa jitihada zao kubwa wanazozifanya za kuhamasisha maendeleo ya Wahadzabe katika maeneo waliyopo ili kuwa na maendeleo endelevu. (*Makofi*)

MHE. MGANA I. MSINDAI: Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Vile vile nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ila akumbuke kwamba na Meatu Wadzabe wapo sehemu ya Sengu. (*Makofi*)

(a) Kwa kuwa hawa watu wanaishi pamoja na kwa miaka mingi wanashirikiana, wakisaidiwa upande mmoja walioko upande wa pili wanahama kwenda kule kwa wale waliopewa msaada. Serikali haioni kwamba sasa kuna umuhimu wa kuanzisha chombo maalum cha kuwasaidia hawa Wadzabe?

(b) Serikali itawasaidia Wadzabe hasa wa Meatu waendeleo kupata msaada kutoka kwa mwindaji aliyeko pori la Makao atoe msaada kwao?

NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:
Mheshimiwa Spika, kwanza suala la chombo maalum kwa ajili ya kusaidia watu wa kabila la Wadzabe nasema tutashirikiana na wenyewe Wabunge wanaotoka katika maeneo haya ili tuone uwezekano wa kuwa na chombo hicho na Serikali iko tayari kusaidiana nao na kuweza kuhakikisha kwamba wanapata maendeleo lakini wanadumisha mila zao.

Pili, kuhusu Serikali kusaidia Wadzabe waliopo katika maeneo ya Meatu ili waweze kufaidika na kampuni inayofanya uwindaji. Ni kweli kabisa makampuni yanayofanya uwindaji kupitia programu ya *Wildlife Management Area* wanakuwa na jukumu la kusaidia kutoa huduma mbalimbali za kijamii lakini vile vile watu wa maeneo hayo wanaweza kupata fursa za utalii wa kitamaduni yaani *Ecol Tourism*. Kwa hiyo, tutashirikiana na Wizara inayohusika, Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuona kwamba kampuni hiyo inayofanya shughuli za uwindaji sehemu za Meatu zinasaidia jamii ya Wadzabe walioko katika eneo hilo. Nashukuru sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nikiri maelezo ya Naibu Waziri ya kina na ni mazuri sana. Pamoja na maelezo hayo, Wabunge na wananchi wangependa zaidi rekodi sahihi kuhusu Wadzabe kwamba Wadzabe wanakaa katika vijiji ambavyo vimeandikishwa na vina hatimiliki. Vijiji ambavyo wanyamapori wanahifadhiwa. (*Makofi*)

Kwa bahati mbaya sana wenzetu walioko Dar es Salaam na Arusha hawawafahamu vizuri Wadzabe na maisha yao hata wakati mwingine kama jana juzi na wanaonyesha picha za Wabarabeig badala ya picha za Wadzabe na ni watu wenye heshima kubwa wanaopigania haki za binadamu ambao wanashindwa kutofautisha baina ya wakazi wa Laeda ambapo Wadzabe wanakaa wakiwa ni pamoja na Wabarbaeig.

Mheshimiwa Spika, yanayoandikwa sasa ni mambo yanayosikitisha kwa sababu kuna wafanyabiashara hasa makampuni ya kitalii, wangependa Wadzabe wabaki walivyo ili wapigwe picha wakiwa katika hali duni sana. Tunaomba wenzetu wa mashirika yasiyo ya Kiserikali watuunge mkono tuinue hadhi na maisha ya Wadzabe bila kudhalilisha utu wao. Ahsante Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Na. 36

Hifadhi ya Pori la Mkomazi

MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza:-

Kwa kuwa pori la Hifadhi ya Mkomazi ni sehemu ya vivutio vya Halmashauri ya Wilaya ya Same; na kwa kuwa ndani ya pori hilo kuna mzungu aitwaye Tony Fitjohn anayeishi humo kwa muda mrefu sasa:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa picha kamili kwa wananchi wa Tanzania kuhusu huyo mzungu kwamba anaishi ndani ya Hifadhi kama mwekezaji au mmilikishwaji na shughuli zake hasa zimeleaga nini ndani ya pori hilo?

(b) Kama Bwana Tony Fitjohn anaishi kama mwekezaji je, mkataba wake ulianza lini na utakoma lini?

(c) Tangu Bwana Tony Fitjohn aanze kuishi katika Pori la Hifadhi ya Mkomazi, je, Serikali imeingiza mapato kiasi gani mwaka hadi mwaka na Halmashauri ya Wilaya ya Same imefaidika vipi na mapato hayo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Bwana Tony Fitjohn ambaye anaishi ndani ya Pori la Hifadhi ya Mkomazi siyo mwekezaji bali ni mwezesaji katika masuala ya uhifadhi endelevu ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali liitwalo *Wildlife Preservation Trust Fund (WPTF)* au kwa lugha ya Kiswahili Mfuko wa Udhadini wa Ulinzi wa Wanyamapori. Fedha za kuendesha Shirika hili zinatokana na michango kutoka matawi ya kimataifa ya *George Adamson Wildlife Preservation Trust Fund* yaliyopo nchini Uingereza, Marekani, Uholanzi na Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Udhadini wa Ulinzi wa Wanyamapori ulikaribishwa na Serikali mwaka 1989 kusaidia kutekeleza malengo yafuatayo kwa pori la Hifadhi ya Mkomazi:-

(i) Kukarabati Pori la Mkomazi kwa kuweka miundombinu.

(ii) Kuendesha programu ya kupandikiza Faru Weusi na Mbwa Mwitu, wanyama ambao wako katika hatari ya kutoweka duniani na ambao walikuwa wametoweka kabisa katika eneo hilo.

(iii) Kuendesha programu za ushirikishwaji jamii katika vijiji vinavyozunguka Pori la Hifadhi ya Mkomazi.

Mheshimiwa Spika, Bwana Tony Fitjohn hajaiingizia Serikali mapato yoyote tangu aanze kuishi ndani ya Pori la Mkomazi. Hata hivyo, amefanya kazi kwa kila lengo lililokusudiwa na Serikali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kukarabati Pori la Mkomazi kwa kuweka miundombinu, kufanya matengenezo na kuweka barabara mpya ndani ya Pori, kusafisha mipaka, kutoa vifaa kwa menejimenti ya Pori.

(ii) Kuendesha programu ya kurudishia faru, wanyama walio katika hatari ya kutoweka duniani. Ujenzi na usimamizi wa eneo la kuhifadhia Faru (*Rhino Sanctuary*) ndani ya Pori la Akiba la Mkomazi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 45 na ununuzi wa faru wanne mwaka 1997 na kisha wengine wanne mwaka 2001. Kati ya hao faru, faru wawili wamezaa watoto jike na dume.

(iii) Uzalishaji wa mbwa mwitu na kurudisha wanyama hao; utafiti wa magonjwa na uzalishaji kwa msaada kutoka Vyuo Vikuu vya Utrecht, Groningen na Rotterdam, Uholanzi. Hivi sasa wapo mbwa mwitu sitini kwenye vituo vitano ndani ya pori.

(iv) Kuendesha programu za ushirikishwaji jamii katika vijiji vinavyozunguka Pori la Hifadhi ya Mkomazi.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hifadhi ya Pori la Mkomazi lipo katika matayarisho ya kuwa Hifadhi ya Taifa hivi karibuni. Hifadhi hiyo ya Taifa tarajiwa ya Mkomazi inategemewa kuunganisha mapori ya sasa ya Mkomazi Mkoani Kilimanjaro na Umba Mkoani Tanga. Hadi sasa Mkoa wa Kilimanjaro umeshatoa ridhaa ya kupandisha hadhi ya Pori la Mkomazi liwe Hifadhi ya Taifa. Kinachosubiriwa sasa ni ridhaa kama hiyo kutoka Mkoa wa Tanga kwa ajili ya Pori la Umba. Ridhaa hiyo inategemewa kutolewa kupitia kikao cha *RCC*. (*Makofi*)

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa majibu niliyopewa na Serikali ni majibu anayotoa Bwana Tony Fitjohn yeye mwenyewe kupitia *website* yake ambayo mimi nimeingia na ku-*print* kila kitu. Lakini si kwamba kila atakachosema ndicho anachotenda, naomba kuuliza swali.

Kwa kuwa hifadhi ya mbuga za wanyama Mkomazi inazidi kushuka hadhi; na kwa kuwa wanyama waliokuwepo pale sasa wanasogea na kwenda Mbuga ya jirani ya Savo ambayo ni ya nchi jirani, je, Serikali imefanya utafiti wa kina haswa na kujua kwa nini wanyama wanatoka huku kwetu, wakati Tony anaishi pale ndani na wanahamia mbuga ya jirani ambayo iko nchi ya Kenya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Watanzania tuna tatizo moja la kuamini watu weupe na mara kwa mara tumekuwa tunapata hasara na tunakuwa tumeshachelewa, sasa naomba kuuliza, ndani ya mbuga na ndani pori lile kuna uwanja wa ndege ambao ndege inaingia na kutoka, ndege ya Tony inaingia na kutoka wakati wowote, je, Serikali imeweka udhibiti gani haswa wa kuona ndege ile inapoingia inaondoka na vitu gani kutoka kwenye pori lile kubwa lenye rasilimali nyingi sana? Naomba majibu kutoka Serikalini.

SPIKA: Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hajajibu, sijui Mheshimiwa Anna Malecela, wewe ni mweupe au maji ya kunde? (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa amesema majibu yanatolewa na Serikali ni yale majibu yanapatikana katika *website* ya Ndugu Tony Fitjohn na sisi ndio hayo tunayatoa.

Pamoja na kwamba anatoa majibu yake katika *website*, lakini vile vile Serikali inafuatilia katika pori, meneja wa pori ambaye yuko katika hilo pori, kwa hiyo pia taarifa tunazipata kutoka kwa meneja pori la Mkomazi, na vile vile idara ya wanyamapori pia inafika kwa wanyamapori na kufanya utafiti. Ni kawaida kwamba siku hizi huu utamaduni wa kuwa na *website* zinakuwepo, ili kila anayeshughulika anatoa taarifa yake na kuhusu utafiti kwamba wanyama wamepungua katika pori la Mkomazi, kusema kweli wanyama wameongezeka, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba wanyama faru, walikuwa wametoweka kabisa katika pori la Mkomazi, Mbwa Mwitu, walikuwa wametoweka kabisa katika pori la Mkomazi lakini sasa tunao faru 10 katika pori la Mkomazi na tunao Mbwa Mwitu 60 katika pori la Mkomazi. Hata hivyo ni kweli kwamba baadhi ya wanyama wanatoka pori la Savo kuja pori la Mkomazi na wengine wanatoka pori la Mkomazi kwenda pori la Savo. Wanyama hawajui mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Spika, samahani pia kulikuwa kuna swali kwamba katika pori hilo kuna uwanja wa ndege, ni kweli kuna kiwanja cha ndege, katika mapori yetu mengi ya hifadhi kuna viwanja vya ndege kwa ajili matumizi ya usafiri, kwa hivyo, kile kiwanja kwa uhakika kiko pale kwa sababu za msingi za usafiri na si vinginevyo.

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inaruhusu wazungu kama Tony Fitjohn kuishi na kufanya shughuli zao ndani ya hifadhi na shughuli ambazo haziiingizii Serikali mapato yoyote, ningependa kufahamu ni kwa nini dakika hii tunavyozungumza hapa, ng'ombe wa wananchi wa Tarime 174 na mbuzi 182 na kondoo 74 zinashikiliwa katika.... (*Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hapa tunazungumzia wanyamapori, ng'ombe sio wanyamapori. (*Kicheko*)

Na. 37

Kuwasaidia Akinamama Wakulima wa Mwani

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA aliuliza:-

Kwa kuwa ukulima wa Mwani ni kitega uchumi kwa Taifa letu na asilimia kubwa ya wanaolima zao hilo ni wanawake; na kwa kuwa mradi huo hauna tija yoyote kwa wanawake kwa kuwa bei si nzuri hata kidogo:-

Je, Serikali itawasaidia vipi akinamama hao ili wapate kupunguza ukali wa maisha?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mbunge Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu biashara ya kilimo cha Mwani hapa nchini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo cha Mwani kilianza hapa Tanzania miaka ya 1980 kufuatia matokeo ya utafiti wa wanasayansi wa Tanzania wakiongozwa na Profesa Keto Mshigeni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hadi sasa wapo wakulima zaidi ya 3000 Tanzania Bara wengi wao wakiwa ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, ukulima wa Mwani umekuwa ukiendelea kukua katika maeneo ya ukanda wa bahari ya Hindi kwenye Mikoa ya Pwani, Tanga, Mtwara na Lindi. Takwimu za mwaka 2004 zinaonyesha kuwa uzalishaji wa Mwani zi zaidi ya tani 1,500 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mafunzo yaliyofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii yamebainisha na kutambua kwamba kilimo hicho kina faida kwa wakulima husika hasa baada ya kupata maelezo kutoka kwa wakulima kwamba wengi wao hawakuwa na shughuli yoyote iliyokuwa ikiwapa kipato kabla ya kuanza kilimo cha Mwani. Aidha, wakulima hao waliweza pia kutoa maelezo ya matumizi ya fedha hizo kwa maendeleo ya familia na hata jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Jukumu kubwa la Serikali ni kuzidi kueleemisha wakulima husika kulima na kuvuna Mwani mwingi wenye kukidhi ubora. Aidha, Wizara yangu imeweka mikakati ya kuendeleza kilimo cha Mwani ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mikataba kati ya wakulima wa Mwani na wanunuzi wa zao hilo inaheshimiwa na pande zote.

(ii) Aidha, Serikali inawahamasisha na kushawishi wakulima wa Mwani kujiunga na vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (*SACCOS*) ili wafaidike na mikopo kupitia katika uwezeshaji wa Serikali na watumie mikopo hiyo kujinunulia pembejeo zao badala ya kutegemea mikopo ya pembejeo kutoka kwa wawekezaji. Hii itawapa nguvu wakulima katika kupanga bei badala ya hali ya sasa ya kupangiwa bei na wanunuzi wa zao hilo. Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri za Wilaya husika katika kuhimiza uundwaji na uandikishwaji wa vyama hivyo vya wakulima wa mwani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inamshukuru Mheshimiwa Mbunge kuliuliza suala hili zuri. Aidha, tunazishauri Halmashauri za Wilaya na Waheshimiwa Wabunge wahimize kilimo bora cha Mwani na kuhakikisha kuwa mikakati ya kuendeleza kilimo hicho ni pamoja na kujiwezesha kupata mikopo ya kununulia pembejeo na kujikwamua kutokana na mikopo ya wanunuzi yenye riba za juu sana. (*Makofi*)

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika moja ya sehemu inayolima Mwani kwa wingi ni Wilaya ya Mafia na bahati nzuri Wizara ya Maliasili ya Utalii mwaka 2003 iliwahi kufanya mkutano wa pamoja wa wadau wa Wilaya zote

zinazolima Mwani Tanzania Bara na Visiwani na mkutano ulifanyika Bwawani, Zanzibar. Mategemeo ya mkutano huo ilikuwa ni kuboresha Mwani kwa kuongeza uzalishaji na kupandisha bei kwa ajili ya zao hilo. Lakini mpaka dakika hii zao la Mwani bei ni shilingi 100 mpaka 220 na kazi yake kubwa.

Sasa nauliza, je, Serikali baada ya kupitia kikao kile, nini madhumuni na mikakati gani zaidi ya kuhakikisha kwamba kutoka tani 1,500 zinazolimwa sasa hivi kutoka mwaka 1980 hadi leo zipo vile vile na wadau wanunuzi wa zao hilo wanasema itakapofika tani 2,500 watakuwa tayari kuanzisha kiwanda kitakachosindika zao hilo hapa hapa na kuongeza bei kwa zao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha zao hilo ili tija iweze kuongezeka kwa wakulima hao?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Maliasili na Utalii ilifanya mkutano mwaka 2003, ikawashirikisha wakulima wote wa Mwani Tanzania Bara, Zanzibar pamoja na wawekezaji na lengo kwa kweli ilikuwa kuboresha ulimaji wa Mwani, ili mkulima wa Mwani aweze kupata tija katika kilimo cha Mwani, ni muhimu awe na kamba zaidi ya 90 zenye urefu wa zaidi ya mita mia mbili kwa kila kamba, ndipo kwa kweli uzalishaji utakuwa na tija. Mpaka sasa wakulima wetu wengi wanaozalisha Mwani wanatumia kamba chini ya 90 na zenye urefu chini ya mita 20. Kwa hiyo, naomba kwa kupitia Bunge lako Tukufu nitoe wito kwa walimaji wa Mwani kuzingatia kwanza ubora wa Mwani na kuzingatia kiwango cha kuzidisha kamba 90 zenye urefu zaidi ya mita 20 kila Kamba. *(Makofi)*

Kuhusu bei, mpaka sasa wawekezaji hao wao ndio wanatoa bado pembejeo kwa wakulima, nimejibu katika swali la msingi kwamba ni vema wakulima wa Mwani waanzishe vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa ili waweze kujinunulia pembejeo zao wenyewe na hata hivyo Serikali bado inaendelea kushughulikia suala la kuongeza bei ya huu Mwani. Wawekezaji wako tayari kuweka viwanda vya kutengeneza mazao kutokana na Mwani, lakini kwa kuwa bado Mwani unaozalishwa ni mchache, ili kiwanda kiweze kujiendesha kibiashara ni muhimu pawe na zaidi ya tani 7,000 kwa mwaka ndipo viwanda hivi vitaweza kuanzishwa. *(Makofi)*

Na. 38

Kiwanja cha Michezo - Moshi Mjini

MHE. PHILEMON NDESAMBURO aliuliza:-

Kwa kuwa kiwanja cha michezo Moshi maarufu kwa jina la *Memorial Stadium* kilianza kujengwa kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita na wananchi wa mkoa walichangishwa fedha ambazo yamkini zingeweza kujenga kiwanja hicho kufikia kiwango cha kuweza kutumika kwa michezo ya humu humu nchini na kuipatia Serikali mapato; na kwa kuwa katika mchakato wa ujenzi wa kiwanja hicho wananchi walipewa nafasi ya kumiliki vyumba vya biashara katika uwanja huo kwa sharti la kujenga ukuta kwa sehemu kubwa ya ukuta wa uzio wa uwanja huo; na kwa kuwa eneo la uwanja huo ni kubwa kuliko eneo lolote la uwanja wowote ulioko Tanzania na kwamba uwanja huo umesanifiwa kuweza

kutumika kwa michezo mingi na kukamilika kwake kutasaidia sana kuendeleza michezo katika mkoa wa Kilimanjaro na kwa kanda nzima ya Kaskazini ambayo haina uwanja mkubwa wenye hadhi ya Kimataifa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiendeleza kiwanja hicho na kukifanya kiwe cha kisasa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutokijenga na kukifanya kiwanja hicho kitumike inadhoofisha nguvu za wananchi zilizotumika katika ujenzi wa awali?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kuanzia miaka ya 1970, mikoa kwa kuhamasisha wananchi, imekuwa ikijenga viwanja katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Pale wananchi walipohamasishwa vizuri na usimamizi wa rasilimali (fedha na watu) zikatumika vizuri, kumekuwa na matokeo mazuri kwani vipo viwanja vizuri vinavyotumika kwa maendeleo ya Mikoa na Wilaya husika. Viwanja vilivyoko Mikoani na Wilayani, cha Moshi kikiwa kimojawapo, imekamilika katika viwango tofauti kutegemeana na jitihada za mkoa au wilaya husika. Aidha, Mikoa ambayo viwanja vyake havijakamilika inaendelea kukamilisha na mingine inafanya ukarabati ili viwe viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

Napenda kusisitiza kuwa viwanja vya mikoa vinajengwa kwa nguvu za mikoa yenyewe na siyo Serikali. Serikali mpaka sasa inajihusisha na ujenzi wa eneo Changamani (*complex ground*) lililoko Dar es Salaam ambapo vinajengwa viwanja vya Taifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ili kuukamilisha uwanja wa Moshi, ninawashauri viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro, akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Mjini wafanye tathmini ya kilichotokea na wajipange upya, wajenge uwanja wa kumbukumbu ya Mashujaa (*Heroes Memorial Stadium*) kwa faida na maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro. (*Makofi*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu ya umuhimu wa viwanja hivi ambavyo vimesambaa katika nchi nzima, vingi vikiwa havijakamilika kama hicho cha Moshi, viwanja hivi ni vya wananchi, lakini mmiliki aliyepewa ameshindwa kuviendeleza, Serikali inasema nini kuvikamilisha kiwanja cha Ali Hassan Mwinyi na kiwanja cha *Lake Tanganyika* kule Kigoma?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA): Mheshimiwa Spika, ni kweli alichosema kwamba viwanja vingi kikiwemo Ali Hassan Mwinyi - Tabora, CCM Kilumba - Mwanza, Kamabarage -

Shinyanga, Jamhuri - Dodoma, *Lake Tanganyika*, Majimaji na viwanja vingine, hivi ni viwanja ambavyo vimejengwa na wananchi wenyewe kwa kuhamasishwa. Ni jukumu la kila Mkoa au kila Wilaya kuendelea kuhamasisha wananchi wake viwanja hivyo wavikamilishe. Sisi kama Serikali katika sera tunao mkakati na tunayo idara maalum ya miundombinu ya viwanja inayosaidia kukarabati viwanja na kiutaalam hasa kuifanya ili viwe na hali nzuri kiutaalam.

Kwa hiyo, ni ombi langu na niiombe mikoa yote ambayo wana viwanja hivi ikiwemo ambavyo amevizungumza Mheshimiwa Mbunge vya *Lake Tanganyika*, wananchi wajipange upya, kuna baraza la *RCC* wakae ili waweze kuweka mkakati kuwa ni *project* mojawapo katika mkoa au wilaya kujenga viwanja. Lakini tukitegemea Serikali ijenge kila kiwanja, kujenga kiwanja ni ghali sana, mfano kiwanja ambacho kinajengwa Dar es Salaam sasa hivi cha Taifa, gharama yake ni bilioni 65 aina ya viwanja vile, kwa hiyo, ni ghali sana kujenga kiwanja, lakini kama Mkoa utajipanga na Wilaya watajipanga, Serikali itaingilia kati kusaidia, ikiwa tayari wao wameshaanza.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu kwamba viwanja hivi vilijengwa kwa nguvu ya wananchi, lakini katika Bunge lililopita walisema viwanja vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi, kwa nini viwanja hivi visiwe mali ya wananchi wote wa Tanzania? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA): Mheshimiwa Spika, ni kweli nilizungumza na ukweli ulivyo kwamba viwanja hivi vyote, mwenye hatimiliki ni Chama cha Mapinduzi, lakini matumizi ya viwanja hivi ni vya wananchi wote. (*Makofi*)

Na. 39

Hali ya Utamaduni wa Tanzania

MHE. AME PANDU AME aliuliza:-

Kwa kuwa kila nchi duniani ina utamaduni wake; na kwa kuwa utamaduni ni kielelezo cha kila nchi duniani:-

(a) Je, utamaduni wetu wa Tanzania unamomonyoka au unaimarika?

(b) Kama utamaduni wetu unamomonyoka, je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuuimarisha?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kila nchi duniani ina utamaduni wake na kwamba utamaduni ni kielelezo cha kila nchi duniani.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kinachomomonyoka sio utamaduni, bali kwa kiasi fulani ni maadili ambayo ni taratibu zinazokubalika ndani ya jamii kwamba zinafaa kufuatwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Idara yake Maendeleo ya Utamaduni imejizatiti katika kutoa elimu kuhusu amali mbalimbali za utamaduni wetu na kuhamasisha hasa vijana juu ya maadili mema, utu bora, kujitambua, kujithamini na kuthamini kilicho chao. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni imekuwa ikihimiza ufundishaji wa masomo ya fani za sanaa, maarifa, uraia na historia ya nchi yetu kuanzia elimu ya msingi hadi vyuoni ili kuwajengea vijana misingi imara ya utamaduni, utaiifa na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ningependa kutoa wito ufuatao:-

(i) Kwanza kabisa, kwa wazazi na wananchi wote hapa nchini; lazima waone umuhimu wa kutambua kwamba ni jukumu la kila mtu kutoa malezi bora kwa watoto na vijana wetu. Hivyo jukumu la kulinda na kuenzi utamaduni wetu lianzie ngazi ya familia.

(ii) Pili, napenda pia kutoa wito kwa vyombo vya habari vyote hapa nchini, visaidie katika kutoa elimu ya maadili mema kwa jamii yetu.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa kuwa suala la maadili linaanza toka nyumbani ambako mtoto analelewa, lakini hivi sasa kutokana na hali ya mwenendo inafikia hali mtoto yule kufikia hadi kushitaki na mzee kushitakiwa kwamba wakati anamrekebisha mtoto wake, je, hali hii utahisi kwamba kweli watoto wetu wanaweza kupata maadili?

SPIKA: Nilipenda pia nitamke kwamba Mheshimiwa Daniel Nsanzugwank,o ni mpya katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO): Mheshimiwa Spika, nashukuru, tunapozungumza kwamba maadili kwamba yaanzie kwenye familia ni utamaduni wa kawaida tu kwamba katika jamii za kiafrika, malezi ya mtoto yanaanzia kwenye familia.

Mheshimiwa Spika, sasa hii dhana kwamba mtoto anaweza kumshitaki baba kwa makosa kadha wa kadha, hayo ni maendeleo na hali inatukumbusha kwamba kinababa na akinamama tuna haki, tunahaja kabisa ya kuheshimu haki y a watoto wakiwa katika familia zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafikiri ni hoja ya msingi tu kwamba familia, baba na mama tuendeleo kuheshimu haki za watoto hawa ambao pamoja na hayo kwamba tumewazaa lakini wana haki zao za msingi ambazo zimetamkwa katika matamko mbalimbali ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, suala la kuheshimu maadili ya watoto ni suala la msingi sana katika familia zetu. (*Makofi*)

Na. 40

Ufufuaji wa Vyama vya Msingi

MHE. ALOYCE B. KIMARO aliuliza:-

Kwa kuwa ushirika ni chombo muhimu cha kupambana na umaskini kwa kuunganisha nguvu za wananchi:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kufufua Vyama vya Misingi katika Jimbo la Vunjo na nchi nzima kwa ujumla ili viendane sawa sawa na uanzishwaji wa *SACCOS*?

(b) Je, *KNCU* inafanya biahsara kwa faida; na kama inapata faida ni kiasi gani na Serikali imechukua hatua gani?

(c) Je, tunavyo vyama vingapi vya mikoa, na je, vinafanya kazi kwa faida, na kama vinapata hasara ni kiasi gani cha hasara hiyo na kama vinapata faida ni kiasi gani cha faida hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID MATHAYO DAVID) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Aloyce Kimaro, kwamba Ushirika ni chombo muhimu katika kuunganisha pamoja nguvu za wananchi kwa lengo la kuondoa umaskini na kuinua hali zao za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini kuwa Ushirika nchini umezorota na haukidhi mahitaji ya wanachama na wananchi kwa ujumla Serikali katika jitihada zake za kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

(i) Imeboresha Sera ya Maendeleo ya Ushirika, imeweka Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake;

(ii) Imerekebisha Sheria ya Shirika la Uchaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*);

(iii) Imepandisha hadhi ya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara kwa lengo la kuimarisha usimamizi na elimu katika Vyama vya Ushirika vya aina zote nchini; na

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau a Ushirika imeanzisha programu kabambe ya mageuzi na modenaizesheni ya Ushirika nchini (*The Cooperative Reform and Modernization Program-CRMP*) ambao ni mpango mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 unalenga katika kuondoa matatizo sugu yanayokwamisha maendeleo ya ushirika nchini na kuwezesha kuwa na mfumo wa ushirika ambao msingi wake ni wanachama katika Vyama vya Ushirika vya Msingi na kuwa na Viongozi wa Ushirika wanaowajibika kwa wanachama na ambao ni wabunifu kibiashara. Pia kwa nia ya uhamasishaji, uanzishaji Vyama vya Ushirika vya Msingi imara na vinavyojibu mahitaji ya kiuchumi ya wananchi wake.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu ya 2003 hadi 2005 Hesabu zilizokaguliwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha *KNCU* zinaonesha kuwa mwaka 2003 chama kilipata hasara ya shilingi 331,326,620.00, mwaka 2004 kilipata faida ya shilingi 146,880,139.00 na mwaka 2005 kilipata faida ya shilingi 319,495,422.00. Mwelekeo huu unaonyesha kuendelea kuimarisha kwa shughuli za chama kunakotokana na juhudi za serikali za kuimarisha Ushirika nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, muundo wa Vyama Vikuu vya Ushirika nchini haulazimishi vyama hivyo kuwa vya Mikoa au Wilaya bali maeneo yake hutegemea aina ya shughuli inayofanyika. Hadi tarehe 30 Juni, 2006, vilikuwepo Vyama Vikuu vya Ushirika 35 ambapo kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2004, Vyama Vikuu tisa kati ya hivyo vilipata faida, Vyama hivyo ni *NCU* cha Kagera, *KNCU* cha Kilimanjaro, *WETCU* cha Tabora, *CETCU* cha Singida, *RIVACU* cha Manyara, *ISAYULA* cha Mbeya, *TDCU* cha Tanga, Usambara cha Tanga na *KACU* cha Shinyanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa orodha inayoonyesha kiasi kamili cha faida au hasara kwa vyama vyote ni ndefu, naomba niwasilishe kwa Mheshimiwa Mbunge kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoeleza katika kipengele (a) cha jibu langu, Serikail kupitia Wizara yangu itaendelea kusimamia mageuzi ndani ya Ushirika ili kupambana na matatizo sugu yanayokwamisha maendeleo ya ushirika nchini kwa kusimamia Sera ya Ushirika na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 ambayo inaweza kusisitiza kwenye suala la ukaguzi wa mara kwa mara wa Vyama vya Ushirika pamoja na kuwa na uongozi imara unaowajibika. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha lakini ninayo matangazo yafuatayo: Kwanza ni wageni. Ninafurahi kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, kutoka Zanzibar. Hakuwataja ni wageni wa aina gani kama ni Madiwani lakini basi nawaomba wasimame pale walipo, wala hawapo sasa. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatambulishe kwenu Wanafunzi wa Shule ya Sekondari kutoka Jimbo la Busega ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dr. Rapahel Chegeni wanaongozwa na Bwana Msoka na Bwana Ibambasi, ni wanafunzi 26 kutoka Busega na walimu wao wawili na pia wana wataalam wawili kutoka nje wanaitwa Kitt na Ruth naomba wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Particular thanks to Ruth and Kitt who are doing volunteer work in our country, we are grateful for your work here in Tanzania, please sit down. (Makofi)

Natumaini Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, hatasema tena nawathamini watu weupe, nathamini kazi yao kwa sababu si rahisi vijana kama hawa kuja na kuishi katika mazingira yetu wakifanya kazi za kawaida kabisa miongoni mwa Watanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wanafunzi 40 kutoka katika shule ya Mwalimu J. K Nyerere, Dar es Salaam. Loh! hawa wamekuja kutoka mbali kweli kweli, lakini pia wanafunzi hawa wanao walimu wao, naomba wasimame wanafunzi hawa wa Mwalimu J. K Nyerere. Karibuni sana na tunawapongeza walimu kwa kuwaleta vijana kuona jinsi demokrasia ya nchi yetu inavyofanya kazi. Nitamke tu hapa kwamba kabla Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Mwantumu Mahiza hajaingia katika siasa ndiye aliyekuwa Mkuu wa Shule hiyo ya J.K Nyerere, ketini na ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo pia wanachuo wa Chuo cha Ushirika Moshi, Spika na Katibu wa Bunge wa Bunge la Chuo ambao ni wageni wa Mheshimiwa Philemon Ndesamburo. Kwa hiyo, hawa nao wana utaratibu kamili wa kidemokrasia katika Chuo cha Ushirika Moshi, naomba wasimame lakini pia namwomba Spika mwenzangu apunge mkono kwanza ili aonekane na Katibu pia. Hongera sana ninyi mmeanza kufanyia mazoezi mambo haya karibuni miaka ijayo badala ya kukaa kwenye *gallery* mnaweza kuwa na fursa ya kuwa katika ukumbi hapa ndani kama Wabunge. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila ambao hakutamka ni wageni wa aina gani lakini naomba wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila popote walipo wasimame, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo lingine ni kwamba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kuna mwenzetu mmoja alikwenda Benki ya Taifa ya Biashara na akasahau nyaraka muhimu huko huko, nyaraka hizo kwa bahati nzuri zimeangukia mikononi mwa Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, ambaye yupo tayari sasa kumrejeshea yeyote anayehusika. Lakini Mheshimiwa Manju Omar Msambya nadhani zina majina au pengine hazina majini lakini basi yeyote yule aliyepoteza nyaraka hizo anaweza kumwona Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri nitamke hapa kwamba miongoni mwetu waliteuliwa Wabunge kuingia katika Kamati kuhusu maoni ya Shirikisho linalotarajiwa la Afrika Mashariki, Wabunge hao ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, CCM, Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, nimemruhusu leo Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa avae makobazi kwa sababu

anaumwa kidole. Kwa hiyo, mkimwona hivyo si kwamba anapendelewa, pole sana vinginevyo ungekuwa umevunja kanuni kwani kwa mavazi hayo ukivaa makobazi ungekuwa umevunja Kanuni, lakini nimekuruhusu na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto. Niliona ni vema niweke kwenye *record* kwa sababu wenzetu wanatuwakilisha katika zoezi maalum hili liliagizwa na Serikali. (*Makofi*)

Katibu, tuendeleo na hatua inayofuata.

UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE: Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI): Muongozo wa Spika

SPIKA: Katibu hata mimi sikukusikia

ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE: Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika la Mashariki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa zoezi hili litahusu watu wasio Wabunge waingie humu ndani lakini kwa mujibu wa Kanuni haiwezekani tukafanya hivyo bila kutengua Kanuni ili wageni waingie ndani ya Bunge kwa sababu watakapokuwa wanajitambulisha tayari watakuwa mbele yetu hapa kwenye Bunge. Sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu lazima tutengue Kanuni ili hilo zoezi liweze kufanyika kwa ufanisi.

Pili, nitangaze kwamba pamoja na hayo kabla ya kupiga kura tutazingatia akidi kwa hiyo, itabidi tuhesabiwe, ningepomba sana utulivu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ikiwa akidi yetu kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 94 kifungu kidogo cha kwanza ni nusu ya Wabunge. Kwa hiyo, kwa taratibu zetu zile za kwenda kunywa chai na kadhalika tusije tukashuka chini ya akidi ambayo ni nusu ya Waheshimiwa Wabunge, itakuwa zoezi zima haliwezi kuendelea kwa sababu hili ni zoezi la kupiga kura na kura zetu kwa ujumla wake zitakuwa zinafahamika na zitakuwa kwenye *record*, kwa hiyo zikiwa chini ya nusu hatutaweza kuendelea. Kwa hiyo, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, aweze kutoa hoja ili tuweze kutengua Kanuni inayohusika kwa mujibu wa Kanuni ya 124.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA KUWARUHUSU WAGOMBEA UBUNGE WA AFRIKA MASHARIKI KUIINGIA BUNGENI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI): Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kutoa hoja kwamba Bunge hili liweze kuwaruhusu wagombea wa Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki waingie

katika Ukumbi huu wa Bunge maana wanaweza kuruhusiwa kukaa kwenye *gallery* lakini kuingia humu ndani ya Bunge ni lazima waombewe kibali maalum na kwamba zile Kanuni zinazozuia watu wa nje zitenguliwe. Kwa idhini yako naomba kutoa hoja kwamba watu hawa wa nje waweze kuruhusiwa kuingia humu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Kwa mujibu wa Kanuni ya 124, Bunge linaombwa sasa liweze kuwaruhusu wageni ambao wana shughuli maalumu kwa sababu hawa ni wagombea wetu tutakaowachagua kwenda kwenye Bunge la Afrika Mashariki na utaratibu unaruhusu tuwasikilize kwa hiyo, tuweze kuwaruhusu kuingia humu ndani. Kwa hiyo, hoja iliyo mbele yetu ambayo naomba muamue ni kwamba tutengue Kanuni kuruhusu wageni hao wainge ndani ya Bunge.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Kanuni ya kuruhusu wageni kuingia ukumbini
ilitenguliwa na Bunge)*

ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa taarifa kama msimamizi wa uchaguzi huu. Nafasi zinazogombewa na vyama ...

SPIKA: Katibu naomba utumie ile *mic* nyingine.

ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE: Kufuatia matakwa ya Kanuni ya 9(a) ya Kanuni ya Bunge ya mwaka 2004 ambazo ndizo zinazotumika kwa hivi sasa utaratibu umewekwa na Bunge hili Tukufu juu ya namna ya kuwapata Wabunge tisa wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka Tanzania kwa mgawanyo ufuatao:-

Kundi A, wanawake wanaohitajika ni watatu, mmoja atoke Zanzibar, Kundi B, Tanzania Zanzibar wajumbe wanaotoka huko ni wawili, Kundi C, hili linagombewa na Upinzani nafasi ni moja, Kundi D, Tanzania Bara nafasi ni tatu. Kama inavyofafanuliwa katika aya ya 11(3) ya Jedwali la tatu la Kanuni za Bunge.

Namba B kwa sasa mchanganuo wa idadi ya Wabunge wa Bunge letu ni asilimia stahili ya viti kulingana na viti tisa vinavyohitajika ni kama ifuatavyo:-

Wabunge wa Upinzani waliopo humu ndani ni 45 ambayo ni sawa na 14.12% ya Wabunge wote, hawa wanastahili viti au kiti 1.2 kwa viti katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Wabunge wanawake jumla yao ni 97 ambao ni sawa na 30% ya Wabunge wote hawa wanastahili viti 2.7, sasa hawa wametengewa viti vitatu.

Wabunge wa Zanzibar jumla yao ni 65 ambao ni sawa na 20.38% ya Wabunge wote na wanastahili viti au kiti kimoja 1.83% ambayo ni sawa sawa na viti viwili na Wabunge wa Tanzania Bara jumla yao ni 255 ambao ni sawa na 79.94% ya wabunge wote, hawa wangestahili viti 7 lakini wametengewa viti vitatu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia saa 10 jioni tarehe 31 Oktoba 2006 ambayo ndiyo ilikuwa siku ya mwisho ya uteuzi nilikuwa nimepokea majina 30 ya wagombea kutoka Vyama vya CCM, CUF, CHADEMA, TLP na UDP. (*Makofi*)

Majina ya wagombea na makundi yao ni kama ifuatavyo, Kundi A ni hawa wafuatao, Maufudha Ali Hamid , Septuu Mohamed Nassor, Janeth Deo Mmari, Janeth Zebedayo Mbeni, Hulda Stanley Kibacha, Dr. Thereza Luoga Havisa, Slyvia Kate Kamba, Dr. Rose Lylian Maeda wote ni kundi A la Wanawake kutoka CCM.

Kundi la Tanzania Zanzibar yaani Kundi B ni hawa wafuatao, Remidius Kisassi, Dr. Said Gharib Billal, Isaac Abraham Sepetu, Abdallah Ali Hassan Mwinyi, Dr. Makame Ali Ussi na Nassoro Juma, wote kutoka CCM.

Kundi la Vyama vya Upinzani yaani Kundi C ni hawa wafuatao, Victoria Sarah Mwanjisi, TLP, Meja Jesse Jeremiah Makundi, TLP, Dr. Mutamwega B. Mugaiwa, TLP, Dr. Fortunatus Lyamtika Masha, UDP, Profesa Mwesiga Laurent Baregu, CHADEMA, Profesa Abdallah Jumbe Safari, CUF na Mohamed Abdallah Rahman Dedes, CUF.

Kundi D ni kundi la Tanzania Bara ni hawa wafuatao, Godlucky Joseph Ole Madee, Dr. Didas John Massaburi, Evod Mmanda Herman, Dr. George Francis Nangale, Profesa Samuel Mwita Wangwe, Dr. Norman Adamson Sigalla, Dr. Richard Simon Kasungu, Dr. Aman Walid Kaborou na Dr. Hadly Mpoki Mafenga kutoka CCM.

Mheshimiwa Spika, upigaji wa kura, kutakuwa na karatasi moja ya kura kwa kila kundi, karatasi hizo ambazo chini yake kuna maelezo ya idadi ya kura zinazotakiwa kupigwa kwa kuweka alama ya vema pembeni ya jina ambalo ndilo chaguo la mpigakura.

Wagombea watakuja mmoja mmoja kwa kufuata *alphabet* ili kujitambulisha, kujieleza na kuomba kura mbele ya Bunge kwa muda usiozidi dakika tano kama itakavyoelekezwa na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, lugha itakayotumika ni ile ile itakayotumika katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani kiingereza. (*Makofi*)

Kundi moja likimaliza kujieleza kura zitapigwa na wagombea wa kundi linalofuata wataanza kujieleza.

Zoezi la kuhesabu kura litashuhudiwa na mawakala kwa aina na idadi itakayoainishwa na Mheshimiwa Spika.

Baada ya zoezi la kura kumalizika Bunge litasitishwa kwa muda utakaoamuliwa na Mheshimiwa Spika, labda kwa taarifa zaidi ni kwamba Waheshimiwa Wagombea tumewawekea chumba ambapo watakaa na huko watakuwa wanaitwa mmoja mmoja kama nilivyoeleza kuja kujieleza mbele yenu.

Hapa ni mwisho wa taarifa yangu kama msimamizi wa uchaguzi huu. *(Makofi)*

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Subiri, tutakwenda taratibu nawahakikishieni uchaguzi utakuwa mzuri kwa hiyo wote tutulie. Ninayo ya kusema yafuatayo, kwanza, uchaguzi huu unaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni ndogo tulizozitunga humu Bungeni kushughulikia uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki na chini ya Kanuni ndogo hizo msimamizi mkuu wa zoezi zima la kupiga kura ni Spika chini ya kifungu kile cha 11(1)(1) *The Voting shall be conducted under the General Supervision of the Speaker.*

Lakini la msingi zaidi ni kwamba uchaguzi huu unaendeshwa Bungeni kwa ujumla utaendeshwa na Kanuni za Bunge kwa maana hiyo kadri tunavyokwenda maamuzi ya Spika yanalifunga Bunge, anayekuwa na tatizo afuate taratibu ni dhahiri kwamba watu wengine watataka kupata mwongozo wa Spika nami nitautoa kwa wakati muafaka lakini baada ya hapo nikishautoa mwongozo ndiyo tutaendelea.

Sasa anayeona haridhiki itabidi afuate Kanuni na kukata rufaa kwa Kamati ya Kanuni kama zinavyosema Kanuni zetu, sasa Kamati ya Kanuni chini ya Mheshimiwa Naibu Spika wakikaa pamoja ndiyo wanaweza kuamua kama mwongozo wa Spika ulikuwa sahihi au lah! Nitahadharishe tu kwamba katika hatua hiyo nadhani kura tutakuwa tumekwisha piga, kwa hiyo labda itasaidia kwa *record* baadaye. *(Makofi)*

La pili ninalotaka kusema ni kwamba hapa leo tunapiga kura kuwapata Wabunge tisa kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakao liwakilisha Bunge hili au nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki kama alivyosema Katibu wa Bunge, uwiano wa kuwapata hao tisa umeelekezwa kutokana na ushindi wa kura kwa Wabunge ndani ya Bunge hili kwa mujibu wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na uwiano amekwisha utaja. *(Makofi)*

Kutokana na uwiano huo kundi la Upinzani linapeleka Mbunge mmoja na Chama cha Mapinduzi kinapeleka Wabunge nane, hakuna tafsiri yoyote nyingine ambayo itatulazimisha tuingie katika kubadili hilo, ni nje kabisa ya uwezo wa Bunge kwa sababu huo ndiyo uamuzi wa wananchi.

Kwa hiyo hakutakuwa na tafsiri ya makundi tofauti na hiyo kwa sababu dawa iko kwa wananchi na hapa ndivyo tulivyo basi uwiano uko hivyo hivyo kwa hiyo, ile tisa tunaigawa kwa mujibu wa jinsi wananchi walivyopiga kura. *(Makofi)*

Baada ya hayo niliona Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ana hoja, kwa hiyo sasa namruhusu.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kifungu cha 55(3) Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tangazo alilotoa Katibu ambaye ndiye msimamizi wa uchaguzi huu na ndiye *Returning Officer*, chama changu kiliwasilisha majina matatu kugombea nafasi katika makundi mbalimbali kama ifuatavyo, jina la kwanza lilikuwa ni la Mheshimiwa Profesa Safari kwenye kundi la *Opposition*, pili ni Mheshimiwa Dedes katika kundi la Zanzibar na tatu ni Mheshimiwa Rekesh katika kundi la Bara ambaye hatimaye kabla ya wakati wa kurudisha fomu yeye alilotoa jina lake na hivyo kubaki wagombea wawili.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Wananchi (*CUF*) kilifanya hivyo kutokana na mwongozo ufuatao ambao ulitolewa katika uchaguzi uliopita wa mwaka 2001 kama ifuatavyo, Ibara ya 11 (3) kulikuwa na malalamiko ya Mgombea wa *TLP* ambaye aliomba nafasi ya wanawake katika kundi la wanawake kwa hiyo *Returning Officer* wakati huo ambaye sasa ni Jaji wa Mahakama Kuu alitoa maamuzi yafuatayo, kwamba Ibara ya 11(3) imeonyesha makundi ya wagombea lakini ukiacha Kundi C ambalo limeelekezwa kugombea vyama vya upinzani Kanuni hazijaelekeza endapo nafasi katika kundi A, B na D zingetengewa wagombea wa Chama Tawala tu au vyama vyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kwa vile Ibara ya 13(3) haijawafunga wagombea wa vyama vingine katika makundi A, B na D na kwa kutumia ruhusa ya jumla iliyopo ya Ibara ya 5(3) nimetafsiri makundi haya kuruhusu wagombea wengine zaidi ya Chama Tawala na nimezingatia tafsiri hii hususan wa kutafakari *form* ya uteuzi ya mgombea wa *TLP* aliyeomba kugombea katika kundi la wanawake Bara. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nimesikia maelekezo yako lakini kwa sababu *Returning Officer* baada ya kupelekewa maombi yetu ya Chama hakuweza kuwasiliana na wagombea wala na chama na akabadilisha maamuzi ya mgombea kinyume cha *Article 17* ya *Second Community* sisi tunahisi uchaguzi huu si halali.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Kwanza uchaguzi hatujaufanya, kwa hiyo hatuwezi kuwa na kitu halali au haramu kabla hakijatendeka, ila mwongozo tu ni kwamba ningepomba Waheshimiwa Wabunge mtazame Kanuni ya 9 yote aliyoyasoma Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed ni Kanuni ndogo zilizoundwa chini ya Kanuni, kuna tofauti kubwa kabisa, kinachotawala ni Kanuni na siyo Kanuni ndogo. (*Makofi*)

Katika *Legal Construction* yaani unaposoma Sheria unatakiwa kwanza uangalie Sheria mama ndiyo maana tunaanza Katiba, Sheria, Kanuni na Kanuni Ndogo mpangilio ni huo.

Waheshimiwa Wabunge sasa Kanuni ya 9(a) ambayo ndiyo inapanga mambo yote ndiyo inatuelekeza kwamba na nitaisoma: “Uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine...” yaani kama huu “...ambavyo kwa mujibu wa Sheria zilizounda vyombo hivyo vinatakiwa viwe na wawakilishi Wabunge na uchaguzi unaofanywa na Bunge wa kuwachagua Wabunge wa Bunge la Afrika umetajwa kabisa kwa kuzingatia kwa kadri iwezekanavyo uwiano wa idadi ya Wabunge wa vyama mbalimbali vya siasa vinavyowakilishwa Bungeni.” (*Makofi*)

Kwa hiyo, kitu cha kwanza ni kuupata uwiano kwanza na ukishaupata uwiano umekwishapata jibu. Kwa uwiano uliopo kama alivyosema *Returning Officer* hivi punde, uwiano uliopo kundi la Upinzani lina kiti kimoja tu kutokana na uamuzi wa wananchi kwenye uchaguzi wa mwaka jana na wala si zamani ni uchaguzi wa mwaka jana tu. Sasa tafsiri yoyote ambayo inapenyeza dhana hii ya msingi ikiukwe ni tafsiri potofu kwa sababu ukisema kundi la upinzani liwepo katika kundi una maana ya kusema kwamba sasa kama uchaguzi ukitokea wakipatikana hata Kambi ya Upinzani watatu hiyo bado ni sahihi ili kupunguza wale walioshinda kwenye uchaguzi, tafsiri ya namna hiyo haiwezekani kabisa na haikubaliki kabisa kwa sababu ni kwenda kinyume cha matakwa ya wananchi, demokrasi ni matakwa ya wananchi.

Nifafanue hapa Kanuni ndogo ziliwekwa katika mfumo ili inapotokea katika chaguzi, nitoe mfano tu ingewezekana kwamba uwiano ukawa tano kwa nne, wapinzani nne na chama tawala watano hapo *formula* ya makundi sasa ingeleta maana. (*Makofi*)

Lakini ukienda tena, sisi Wanasheria tunasema *reducing the argument to absurdity*. Kama chama kimoja chochote kingeshinda asilimia mia moja kwenye uchaguzi wa mwaka jana maana yake makundi yote yangukuwa ni Wabunge wa chama hicho tu. Mnanifuata mpaka hapo? Yaani ikiwa ni asilimia mia moja basi kila kundi iwe ni wanawake, Zanzibar kwa asilimia mia moja maana yake Wabunge wote ambao wangechaguliwa kwenda Bunge la Afrika Mashariki wangukuwa wa chama hicho kimoja. (*Makofi*)

Sasa kilichotokea mwaka jana, kambi nzima ya upinzani imeleta Wabunge ambao wanafikia asilimia 14. Jamani asilimia ingekuwa angalau 20 katika mia, ndio inafikia wawili, 14 haifiki popote. Kwa hiyo, mimi sina njia ila kusema kwamba mwongozo wangu ni kwamba taarifa aliyoisoma Katibu ndio sahihi. (*Makofi*)

Kimahesabu asilimia 14 ya Wabunge tisa tunaotaka kuchagua ni Mbunge 1.2. Wote tumefunzwa toka shule ya msingi kwamba inapokuwa 1.2 haiwezi kupandishwa ikawa mbili. Unapozungumzia binadamu, binadamu 1.2 haiwi. (*Makofi*)

Nimeelezwa hapa kabla mfano wa Uganda ambao Kambi ya Upinzani imetoa wawili. Uwiano kule ni tofauti wao sio 1.2 wamefika 1.57. Ndio Uganda sasa wakasema

basi tuwe na wapinzani wawili. Kwa hiyo, kwa hali hiyo, haiwezekani nikazipinda kanuni au nikapinda hata Katiba ili kuweza kuleta jambo ambalo sio sahihi. *(Makofi)*

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Hakuna taarifa. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaendelea, nimeshatoa mwongozo, unaupinga kwa mujibu wa Kanuni Mheshimiwa, hakuna taarifa hapa, Katibu!

ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE: Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika... *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge wa Kambi ya Upinzani walitoka Ndani ya Ukumbi wa Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, hata hawa waliotoka, hakuna athari yoyote kwa sababu akidi bado tunayo na akidi ndani ya Bunge haitegemei uwakilishi wa vyama. Kwa hiyo, sisi tunaendelea na zoezi hili. Naomba sasa Katibu atangaze hatua zinazofuata. *(Makofi)*

ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa sababu tayari idhini imeshatolewa, naomba sasa wagombea wote waje katika ukumbi huu ili maelezo yaweze kutolewa na baadaye waende katika chumba maalum.

SPIKA: Katibu, nimeona tumepata nafasi ya viti wazi hapa mkono wangu wa kushoto, ili tuutumie ukumbi kwa ufanisi, naomba wale wagombea wakae hapa. *(Makofi)*

(Hapa Wagombea wa Bunge la Afrika Mashariki waliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge na kukaa sehemu waliyopangiwa)

SPIKA: Karibu sana Waheshimiwa Wagombea, kuna nafasi bado kwenye viti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wagombea, naomba mjaze viti hivi hapa, mkichanganyika na Waheshimiwa Wabunge huko mtanipa taabu, mstari wa mwisho ni huu hapa, bado viti tele mpaka nyuma pale. Waheshimiwa wetu wagombea wa viti vya Bunge la Afrika Mashariki, kwa niaba ya Bunge napenda kuwakaribisheni sana ndani ya ukumbi huu. Sasa hivi, bahati njema wakati Katibu anasoma Kanuni zinazotawala uchaguzi mlisikia mkiwa pale kwenye *gallery*. Wajibu wangu sasa ni kuwaeleza kwa undani utaratibu wa kuanzia hapa sasa. Nimeamua kwamba kila mgombea ataingia hapa kwa mujibu wa *alphabet* kulingana na kundi, tuna makundi manne. Yale makundi yetu manne, Kundi A la wanawake, kundi B la Tanzania Zanzibar, Kundi C Vyama vya Upinzani na Kundi DTanzania Bara. Kwa hiyo, kila kundi kwa *alphabet* kwa mtiririko huo huo niliokwishausoma.

Mgombea akishaingia hapa ndani kwa hatua ya kujieleza, anapewa dakika tano au muda usiozidi dakika tano, sio lazima uzitumie zote. Ukiona umeeleza kwa kifupi imetosha na nitahadharishe tu, Waheshimiwa Wabunge ninavyofahamu, wanapenda anayejieleza kwa kifupi. Ukishajieleza, kuna fursa ya Waheshimiwa Wabunge kuuliza maswali yasiyozidi matatu, wanaweza wasiulize kabisa, wanaweza wakauliza moja lakini hayazidi matatu kwa ruksa ya Mwenyekiti.

Sasa kanuni za uchaguzi huu zinanipa mamlaka ya kuteua mawakala wangu wa chumba cha kuhesabu kura na nimeona ni vizuri niteue kutoka miongoni mwa watumishi wa Ofisi ya Bunge. Kanuni hazikuzuia Waheshimiwa Wabunge lakini kwa kutenda haki kwa sababu takribani kila Mbunge ukiacha Spika, kila Mbunge ana mtu wake hapa. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nimeona wakala wangu wa kuhesabu kura wawe ni watumishi wa Bunge ambao ni waandamizi. Nao ni Mama Kitolina Kippa, mama Kippa yuko wapi? Ndugu Eliakim Mrema, anyooshe mkono pale alipo, njoo wakuone hapa kwa sababu wana haki ya kukukataa, mama Kippa, sokea wakuone.

(Hapa Ndugu Eliakim Mrema na Ndugu Kitolina Kipa walisogea katikati ya Ukumbi wa Bunge)

SPIKA: Wote hawa ni Maafisa Waandamizi wa Ofisi ya Bunge, wana uzoefu mkubwa sana wa kusimamia mambo haya. Wengine ni Ndugu Oscar Mtenda na Ndugu John Joel.

Hawa ndio Maafisa ambao ni mawakala wa Spika kwa makundi yafuatayo, Mama Kitolina Kippa atasimamia kundi A wanawake, ndugu Eliakim Mrema atasimamia kundi B Tanzania Zanzibar, Ndugu Oscar Mtenda atasimamia kundi C na huyu ni Mwanasheria Mwandamizi ni vizuri aende huko huko kusimamia vyama vya upinzani, Ndugu John Joel atasimamia kundi D, Tanzania Bara. Pamoja na hao, ninao wawili ambao watahusika na kuwasimamia vijana wa kuhesabu kura chini ya usimamizi Ndugu Phoebe Mmbaga, huyu ndiye kiongozi kwa maana ya kuhesabu kura wale ni mawakala wa Spika kuangalia mambo yanakwenda sawa sawa. Ndugu Mmbaga ni mzoefu sana, amekaa zaidi ya miaka 20 katika Bunge hili na Ndugu Kileo Nyambele atasaidiana naye tafadhali kwenye kuhesabu kura. Pamoja na hao kutakuwa na vijana wetu kumi na tano ambao sina haja ya kupoteza muda wa Bunge kuwataja kwa sababu wao ni kama mashine za kuhesabu. Wanisamehe wanavyosikia hivyo hii ni lugha ya kitaalamu tu sio mashine, kwa leo ni mashine ya kuhesabu lakini tunajua ni binadamu na ni watu wazuri tu. *(Makofi)*

Nimalizie lingine, kila mgombea anaruhusiwa katika kipindi cha kundi lake kuteua kwa maana hii sasa mwakilishi nje ya hao, hawa ni wa Spika sasa ambaye anaweza kushuhudia kura zake. Kwa hali ya kawaida, hili litatupa taabu sana kwa sababu Wabunge ningependa wabaki humu waendeleo kupiga kura kwa kila kundi. Sasa mkiwachukua wengine waende huko ndani, itatupa taabu.

Naambiwa nyakati zilizopita wengi waliamini tu kwamba zoezi hili linaendeshwa kwa haki lakini yule anayeona kuna wasiwasi kuhusu zoezi zima, nitamruhusu lakini nitasita sana kumruhusu amchukue Mbunge kwenda huko. Kwa sababu kwa idadi yenu, ina maana tutapunguza Wabunge zaidi ya 30 ili waende kushuhudia au waende wenyewe nadhani.

Zoezi hili linafanywa kwa uwazi kabisa. Kwa hiyo, wagombea mnaweza kupita pale kwa zamu kulingana na kundi lako ndio maana itakuwa wachache wachache ili kuangalia kinachoendelea. *(Makofi)*

Kwa sasa nitawauliza tu kati ya hawa wanaotoka Ofisi ya Spika, kuna mgombea yeyote ana kipingamizi? Mwenye kipingamizi basi asimame hapo alipo nitamruhusu aseme. Naona hamna. Kwa hiyo, nawaruhusu watumishi muweze kurudi, ndugu Kileo Nyambele rudini sasa kwenye sehemu zenu.

(Hapa watumishi wa Bunge ambao ni mawakala wa Spika walirudi kwenye sehemu zao walizopangiwa)

SPIKA: Kabla hatujaendelea na zoezi la kuwaita kujieleza, nataka kutoa fursa kwa mgombea yeyote ambaye ana swali, anataka ufafanuzi, basi nitoe nafasi hiyo ili tutakapoanza twende moja kwa moja. Kuna mgombea yeyote anahitaji ufafanuzi kwa haya tuliyoayasema na aliyoyasema Msimamizi wa Uchaguzi? Naona hakuna. Sasa Katibu waelekeze katika ukumbi ili tuanze ile kazi kwa kuanzia na kundi A ambalo ni kundi la wanawake. Kwa maana hiyo, wafuatao, nadhani Katibu wewe uwasome, sio kazi yangu mimi.

ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, tutaanza na Kundi A na kama nilivyokuwa nimesema mwanzo, orodha yao ni kama ifuatavyo: Kwanza atakuwa Hamid Mahfoudha Alley, atafuatiwa na Dr. Huvisa, Tereza Luoga. Katika karatasi ambayo tumeitengeneza ya kupigia kura tumeweka kwa pamoja na chini tumesema hivi, piga kura tatu tu kwa kundi hili lakini moja mpigie mgombea kutoka Zanzibar. Sasa hawa tumewapanga ifuatavyo, kama nilivyosema wa kwanza ni Ndugu Hamid, Mahfoudha Alley. Kwa sababu tunawapigia kura kwa pamoja, karatasi ni moja, ningependa waje wote wajielezee baadaye mtaamua lakini masharti au maelekezo tuliyoyatoa ni kama niliyoyasema hapo. Halafu atafuatiwa na Dr. Huvisa, Tereza Luoga, baadaye atakuja Kamba, Silvia Kate, baadaye atakuja Kibacha, Hulda Stanley, atafuatiwa na Dr. Maeda, Rose Lilian, atafuatiwa na Mbene, Janet Zebedayo, halafu atafuata Ndugu Mmari, Janet Deo halafu tunamalizia na Ndugu Nassor, Sebtuu Mohamed kutoka Zanzibar. Vile vile tumetoa maelezo ambayo yatakuongoza katika kupiga kura na vile vile haya nitayarudia mtakapopiga kura. Mimi nitawaongoza kwenda huko ila naomba abaki sasa yule wa kwanza ambaye ni Ndugu Hamid, Mahfoudha Alley.

SPIKA: Waheshimiwa Wagombea, basi mtaelekezwa kwenye chumba, abaki, aah, subirini kuna swali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI): Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa ujasiri na umakini uliotumia leo. Leo umekuwa makini kama ulivyo siku zote na kwa kweli maelezo yako tumetosheka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazo langu lilikuwa hapa mwishoni katika utaratibu wa kujieleza. Nilikuwa napendekeza kwamba ni kweli karatasi itakuwa moja ya wanawake lakini ndani ya karatasi ile kutakuwa na Zanzibar na Bara. Lakini nilikuwa naomba sana ingetumika hiyo hiyo karatasi awe nayo pale halafu katika kujieleza uchukue moja, mbili, tatu katika kundi la Zanzibar halafu wafuatie wengine wajieleze. Hii itatusaidia sisi kuweka kumbukumbu kwamba huyu alijieleza kundi la Zanzibar. Kuwachanganya itatuletea tatizo, naomba kutoa wazo hilo.

SPIKA: Hoja hiyo inakubalika. Nadhani ni vizuri iwe hivyo kwa sababu hata Katibu kwenye *ballot* wa kwanza na wa pili ndio Zanzibar kwa wanawake.

WABUNGE FULANI: Aah, aah!

SPIKA: Siyo, ooh, doh! Waheshimiwa Wabunge, naukubali ushauri wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, lakini kwa kuwa *ballot papers* tayari zimechapishwa basi tuwasikilize kwanza wale wawili wa Zanzibar, wako wawili tu, tukishawasikiliza hao, tuendeleo kuwasikiliza wengine, sasa wakati wa kupiga kura mnakuwa tu makini kwamba Zanzibar ni wa kwanza na wa nane yaani wa kwanza na wa mwisho yaani lazima uchague mmoja kati ya namba moja na namba nane ama sivyo kura yako imeharibika.

MBUNGE FULANI: Aah!

SPIKA: Ndiyo! Kwa hatua hii hatuwezi kufanya lingine tutachelewesha sana uchaguzi bure. Wa kwanza na wa nane halafu ndio unachagua wawili kati ya namba mbili na namba saba ili kupata watatu. Nadhani hilo linaeleweka. Haya wagombea sasa tunawaomba mtoke abaki Mheshimiwa Mahfoudha Alley Hamid.

(Hapa Wagombea Ubunge wa Afrika Mashariki walitoka ndani ya Ukumbi wa Bunge kuelekea chumba walichoandaliwa)

SPIKA: Wakati Waheshimiwa Wagombea wetu wanatoka, napenda kwa kuzingatia tu *democracy* na *Hansard* kueleza kwamba wapo Wabunge wa Vyama vya Upinzani ambao wameridhika na wamo humu ndani. Kwa sababu upinzani sio kupinga hata kilicho dhahiri kabisa unapinga tu basi uonekane umepiga. Kwa hiyo, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa (CHADEMA); Mheshimiwa Grace Kiwelu (CHADEMA); Mheshimiwa Susan Lyimo (CHADEMA); Mheshimiwa John Cheyo (UDP); Mheshimiwa Philemon Ndesamburo (CHADEMA); Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya (CHADEMA); Mheshimiwa Lucy Owenya (CHADEMA) na Mheshimiwa Said Arfi (CHADEMA), hawa nane tunaendelea na zoezi hili. Nawakushukuru sana kwa kuonyesha moyo huo, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa mgombea wa kwanza Mahfoudha unaweza kuja kwenye *mic* hapa sasa, hebu washeni ile *mic*. Kwa kuokoa muda, sitakuwa narudia maelezo kwa kila mgombea upya tena, una dakika tano na maswali yasiyozidi matatu.

ND. MAHFOUDHA ALLEY HAMID: *Thank you very much Honourable Speaker. My name is Mahfoudha Alley Hamid. I am the current member of East African Legislative Assembly from Zanzibar women seat. Details briefly are entirely in this list of candidates except for a slight correction, they are all right. Currently I am incumbent member of the East African Legislative Assembly which has not been included here.*

Ndugu Ebot Manda Heryman kura 9, Dr. Richard Simon Kasungu kura 21, Dr. Hadley Mpoki Mwafyenga kura 27, Ndugu Goodluck Joseph Olmedee kura 51, Profesa Samwel Onesmo Wangwe kura 113, Dr. Norman Adamson Sigalla kura 124, Dr. Aman Walid Kabourou kura 130, Dr. George Francis Nangale kura 132 na Dr. Didas John Massaburi kura 157. Waliochaguliwa ni wafuatao: Dr. Didas John Massaburi, Dr. George Francis Nangale na Dr. Aman Walid Kabourou. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo taarifa ya matokeo ya uchaguzi wa Wabunge la Bunge la Afrika Mashariki.

SPIKA: Ahsante sana Ndugu Katibu wa Bunge ambaye pia ni *Returning Officer, order please*. Hayo ndiyo matokeo na kabla sijawaita wagombea walioshinda ambao waliochaguliwa kwa ajili ya shukrani. Ningeomba wagombea hii ni fursa yenu kama kuna yeyote ana neno lolote kuhusu mwenendo wa uchaguzi, hii ndiyo nafasi yake ya kuweza kusema. Kwa hiyo, utasimama hapo ulipo Spika atakuona na nitakuruhusu uweze kusema unalotaka kusema.

PROF. SAMWEL M. WANGWE: Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Aah! Chombo, toa kadi halafu *reinsert and then*, sawa sawa.

PROF. SAMWEL M. WANGWE: Najifunza hivyo. Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba hata wale ambao hawakufanikiwa kama unaweza kuwapa nafasi ya kushukuru kama inawezekana.

SPIKA: Ni wazo zuri. Basi nadhani kwa hiyo ili kuzuia uwezekano wa shamra shamra hapa mwanzo zikachukua nafasi kubwa mno ningeomba kwenye kundi la wanawake ukiacha Waheshimiwa Septuu, Mheshimiwa Janeth Mmari na Mheshimiwa Kate Kamba wale wengine kama wana neno la kusema. Tunaanza na kundi (a). Utaratibu ni ule ule, chomoa kadi irejeshe, bonyeza useme.

ND. ALLEY H. MAHFOUDHA: *Thank you Honourable Speaker.*

SPIKA: Kwa hatua hii mnaweza kuongea hata Kiswahili.

ND. ALLEY H. MAHFOUDHA: *It doesn't matter, I feel comfortable in English if you don't mind. I would like to take this opportunity to thank all the Members of Parliament who voted for me and those who did not vote for me. I feel that democracy has taken its course. And I wish my successor every success in her new job and I wish her good health and opportunities. Thank you very much. I thank you. (Applause)*

SPIKA: Yeyote mwingine anayetaka kuongea. Mheshimiwa Janeth Mbene.

ND. JANETH Z. MBENE: *Thank you very much Mr. Speaker and Honourable Members of Parliament. I would also wish to take advantage of this opportunity to thank all of you for your support, I would like to express that I have received a lot of support from many of you by the way of advice counseling and guidance. And I feel that, trimulate my colleague here, that democracy has taken place here and I really appreciate the whole process the way it went.*

I would like to accept the results and edge all those that has been selected to continue doing the good work that the other have done. I, as an expert in economic integretion and international trade, I am available for any kind of support, be consultancy and I would like to say again thank you very much and good luck and best wishes. (Applause)

SPIKA: *Well said, thank you very much. Kuna neno lolote? Msaidie Mheshimiwa Kibacha pale. Wewe kijana! Page Boy, msaidie, hakuna kadi. Mheshimiwa ameondoka na kadi naona.*

ND. HULDA S. KIBACHA: Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii awali ya yote kabisa kushukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao nimeuona wakati wa kampeni. Kwa kweli mimi nimetiwa moyo sana kwa sababu kila nilipoomba hakuna hata nikiangalia usoni sikuona mtu ambaye amefikiri kana kwamba alikuwa hanipi kura. Lakini haya ndiyo matokeo ya uchaguzi. Niwashukuru kwa kunipatia miezi saba, sasa mmeamua nipumzike.

Kwa hiyo, nawashukuru kwa kila jambo na wale ambao wamechaguliwa pia nawatakia kila la kheri, wale walio wanya, wale walio wa zamani, wanaendeleza yale ambayo yamekuwepo. Pale ambapo itahitajika uzoefu, kwa sababu mimi mzoefu, basi tunaweza tukashirikiana. Nashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Anayefuata Dr. Huvisa. Chomoa irejeshe humo humo halafu bonyesha cha kuzungumzia.

DR. HUVISA T. LUOGA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na *Members of Parliament*. Mimi nasema ahsante sana. Shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na kuwawezesha Waheshimiwa wote kuingia kwenye ukumbi huu na kuonyesha moyo wa upendo. Nasema ahsante kwa ushirikiano.

Lakini mimi binafsi naona nimebahatika kwa sababu unaona hata kutumia hiki kifaa nimejifunza leo. Kwa hiyo, hata kuingia tu ndani ya Ukumbi wa Waheshimiwa ni tuzo. Kwa hiyo, nasema ahsante sana na nitakuwa tayari kabisa kushirikiana na wale wenzetu ambao wamechaguliwa kwenda kutoa mchango wetu *East Africa* nawakaribisha Chuo Kikuu, kwa sababu Chuo Kikuu sisi tunatakiwa kutoa *challenges* za kila siku kama mnavyoona kuna Maprofesa walikuja ambao ni walimu wangu. Kwa hiyo, karibuni sana wakati wowote mnapohitaji msaada sisi tuko tayari ahsanteni. (*Makofi*)

SPIKA: Nadhani sasa tumemaliza kundi (a) ukiacha wale waliochaguliwa. Kwa hiyo, sasa nakwenda kundi (b) tuwasikie wale wengine ukiacha Mheshimiwa Mwinyi na Mheshimiwa Dr. Bilal. Balozi Sepetu.

BALOZI ISAAC A. SEPETU: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wote, mimi nimesimama hapa kwanza kutoa shukrani. Shukrani kwa sababu mwaka 2001 ni Bunge hili hili liliniteua kunipeleka katika Bunge la Afrika Mashariki na safari hii Bunge hili hili limeamua kunipumzisha. Mimi nashukuru hiyo lakini pia nashukuru ushirikiano wote nilioupata wakati wa kampeni na moyo niliopewa katika kuangaika katika kampeni. Mimi nayakubali haya matokeo ni sahihi na hii ndiyo *democracy*. Hivyo kwa moyo mkunjufu kabisa na moyo wa shukurani nakwenda kweli kupumzika kwa sababu pia umri unahitaji hivyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, mwingine.

ND. NASSOR J. MUGHEIRY: Mheshimiwa Spika, ningeomba kutoa shukrani nyingi kwako wewe na kwa Wabunge wote na vile vile kwa chama changu cha Mapinduzi, bila Chama Cha Mapinduzi nisingefika hapa. (*Makofi*)

Vile vile, natoa shukrani kwa wenzangu wote waliofanikiwa na hapa hapajakuwa na mshindi. Sote tumekuja hapa kutaka kutumikia nchi. Kwa hiyo, ni tegemeo langu wataitumikia nchi ipasavyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

ND. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wote, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuruni kwa dhati kwa sababu demokrasia imefanya kazi pamoja na kwamba demokrasia ya nchi yetu bado ni changa. Lakini lazima tuanzie mahala na hapa imeonyesha upevu.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kukushukuru sana wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa msaada na ushauri na mawazo ambayo yamenisaidia kunifikisha hapa nilipofika. Nina hakika basi leo sikushinda siku nyingine nitashinda. Hawa walioshinda nawatakia kazi njema na sisi tuko tayari kushirikiana pamoja ili kuendeleza nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

DR. MAKAME ALI USSI: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, mabibi na mabwana. Kwanza kabisa ninapenda kushukuru utaratibu nzima uliopita wa kufanyiwa kura wagombea wote wa Afrika Mashariki na ninapenda kusema kwamba utaratibu nzima ulikwenda vizuri na umekwenda kidemokrasia na waliostahiki wamepita, ambao hawakustahiki siyo kwamba hawafai isipokuwa tu nafasi ni chache, kwa hiyo walitakiwa wachache. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nashukuru sana kwa mashirikiano ya wenzetu hawa ambao wamepita wakati ule tulipokuwa tunapiga kampeni tulikuwa tunashirikiana kwamba tulikuwa hatujui nani atapita. Kila mahali tulikuwa tunapita wote. Kwa hiyo, pia nawashukuru Wabunge wote mikono ilikuwa mingi wakati mwingine wanachoka kupokea mikono lakini walitustahimilia na wakaweza kutupokea hivyo hivyo na kutuomba dua tuweze kufanikiwa. Nawashukuru wote kwa kura zote za mara mbili, mara ya kwanza wamenipa kura nzuri kabisa na mara hii wamenipa kura nzuri kabisa. Nawashukuru wote ahsanteni. *(Makofi)*

SPIKA: Tumemaliza kundi (b) ukiacha wale washindi ambao watakuwa na utaratibu tofauti. Sasa kundi (c) kundi la vyama vya upinzani. Kuna *Major* Makundi.

MAJOR JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Balozi wetu katika Bunge la Afrika. Mimi nimevutiwa sana na hali ulivyofanyika uchaguzi huu. Nakupongeza sana kwa kusimamia vizuri uchaguzi huu. Nawashukuru sana Wabunge waliopiga kura. Kura nilizopata siyo haba. *(Kicheko)*

Ni namba nzuri ya kuanzia. Nimekuja kujifunza, siku zote majeshi yanakwenda doria kwanza halafu kuja kufanya kazi vizuri baadaye. Kipindi hiki nawatakia kila la kheri wale waliochaguliwa waende kutuwakilisha vizuri kabisa katika Bunge la Afrika Mashariki. Wafanye yale ambayo yanahusu uzalendo kwanza kuliko ubinafsi. Ndiyo hicho kilichonipelekea mimi kujitosa kuja hapa kutafuta huu uzalendo kwanza angalau basi niwe katika hao aliochaguliwa, kuna mtu mmoja anaitwa *Political Militant Major* Makundi hapa, basi niliona labda hapo ndiyo mahali pake pa kwenda na hii timu kamili ya mashujaa wa nane waliotoka kwenye Chama Tawala, Chama Cha CCM.

Hivyo, mwisho tunasema bila kuwachosheni, nawatakieni kazi njema Waheshimiwa Wabunge kila la kheri katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mtekeleze wajibu wenu vizuri hatimaye tutapata mafanikio na maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana *Major* kwa matokeo haya hata Spika hawezi kukudanganya kwamba alikupigia kwamba alikupiga kura. (*Kicheko*)

Tunaendelea. Wakati wa kushukuru Dr. Rose Maeda alikuwa bado hajaingia humu ndani. Ameniletea karatasi kwamba angependa kushukuru. Nampa nafasi Dr. Rose Maeda.

DR. ROSE LILIAN MAEDA: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge. Kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kufikia hatua hii. Hii ni *attempt* yangu ya kwanza ya kisiasa na ninaahidi sitaishia hapo. (*Makofi*)

Nashukuru sana kwa kura zote, nashukuru kwa ushirikiano mzuri nilioupata kati ya Wabunge wote. Nawataki kazi njema, muendeleo kwenda mbele kutetea nchi yetu kwa sababu tunahitaji kutetewa. Mungu awabariki wote, ahsanteni. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Dr. Tunaendelea kwenye kundi hilo la vyama vya upinzani kama kuna yeyote mwingine ambaye kundi (c) anapenda kusema neno! Naona Mheshimiwa Mwanjisi hayupo, Mheshimiwa Profesa Baregu hayupo, Mheshimiwa Mgaywa pia hayupo na wale waliojitoa. Kwa hiyo, kwa kundi hili tumemaliza. Sasa nakuja kundi la mwisho kundi (d) kundi la Tanzania Bara kama kawaida tukiacha wale ambao wamekwishachaguliwa kama kuna yeyote Waheshimiwa wagombea ambaye anataka kusema ama kushukuru natoa nafasi.

DR. HANDLEY M. MAFWENGA: Ahsante Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mimi binafsi najisikia furaha sana kwa sababu nilivyokuwa katika Chama changu cha Mapinduzi nilishika namba 9. Lakini Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limenipa namba 7. (*Makofi/Kicheko*)

Mimi hii naichukulia kwamba ni *challenge* labda pengine nizungumze tu kwamba nachukulia kwamba hii *it is more than politics* tunapozungumzia hii *Legislative Assembly* ya *East Africa*. *It is more than politics*.

Kwa hiyo, nawashukuru sana kwamba mmelijua hilo kwa kuchagua madaktari wenzangu wazuri Mheshimiwa Kabourou, Nangale na Massaburi ambao naamini watakapokuwa wakichapa kazi hawatanisahau kwa sababu kwa muda mfupi huu ambao tumekaa tumeshaafahamiana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, napenda tena niwashukuru wote viongozi wangu, sitosita kuzungumza, Prof. wangu Mwakyusa ambaye ndiyo Mbunge wa Jimbo langu kwa kweli amenisaidia, Prof. Mwandosya amenisaidia sana, lakini ni lazima nizungumze niseme ukweli sio kwa maana ya kuwa na *interest* hapana, kuni-*encourage* kwamba *in the politics* kwa kweli kuna hili nenda, nenda. Lakini shukrani za pekee niseme tu mama kwa kweli nimejitahidi, sikukuangusha kuwa namba saba, nakushukuru sana, narudi Hazina kwenda kuchapa kazi na kuzitekeleza sera hizi hizi za *East Africa*. Kwa hiyo, nina imani

nitazitekeleza hizi sera *at the technicality level* ambapo Wabunge wataweza kwa njia moja au nyingi ku-*share ideas* na mimi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru ahsanteni sana.

ND. OLE MEDEYE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge, naomba nitumie fursa hii kwanza kuwashukuruni nyote, tulikuwa hapa kuanzia Jumamosi iliyopita, tukipita kuomba *support* ya Waheshimiwa Wabunge na napenda kukiri kwamba walituunga mkono kwa kiasi kikubwa sana.

Kupata kura ni jambo moja, kupata yule wa kukufariji na kukutia moyo ni jambo kubwa sana ambalo kila binadamu anahitaji. Hasa wakati ule kwamba unafadhaika ukitafta kufikia lengo ulilonalo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwa ruhusa yako niwashukuruni nyote Waheshimiwa Wabunge kwa kuniunga mkono katika hatua hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili naomba niwapongeze wenzangu wale ambao wameteuliwa na Bunge hili kutuwakilisha, nilipokuwa nikijieleza niliomba, naomba mnifanye sehemu ya timu itayokwenda ikiwa mtaona inafaa. Sasa naamini kabisa kwamba hao waliochaguliwa ni timu ya Tanzania na tunaamini watacheza ipasavyo ili kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa letu yanalindwa na sisi ambao tunapata fursa ya kushiriki kwenye mikutano ya Maafisa Waandamizi wa Afrika Mashariki, tutajitahidi sana kuwasaidia kadri inavyowezekana kwa kuzingatia taaluma zetu na maeneo tunayofanyia kazi. Nazidi kuwashukuruni na nasema kuvunjika kwa koleo sio mwisho wa uhunzi. Tutaendelea katika mchakato huu, ahsanteni sana.

MHE. PROF. SAMWEL M. WANGWE: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, mmenipa kura nyingi kweli kweli ingawaje hazikutosha na hazikutosha kwa sababu mlikuwa na timu kali kabisa, uchaguzi najua mlipata kazi ngumu sana kuchagua kati ya watu wakali hawa wote ni *first eleven*, lakini ilibidi, *round* ya kwanza ya kucheza iwepo na wengine tutakuwa ma-*reserve*, tunaamini kwamba katika kipindi chote hiki hakuna atakayeumia.

Kwa hiyo, ma-*reserve* tuvumilie tu, mpaka *round* nyingine ambayo tutakuja tena. Tunawahakikishia kwamba hii sio mara ya mwisho, kuna mtaalamu mmoja alikuwa ananishauri kuwa unajua kwenye siasa ukishaonja hivi, kurudi nyuma ni vigumu sana, utarudi tu! Nikambishia, lakini naamini kwamba tutaonana *in other capacities* na kwa wale wenzangu ambao Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limechagua kuwapeleka kule, mkumbuke kwamba kule mtakuta mpango wa miaka mitano ambayo mimi na timu yangu tulitayarisha. Kwa hiyo, mkikwama popote pale mimi niko *available* kuweza kutoa ushauri. (*Makofi*)

Natoa usia kwamba, sasa tunaingia kwenye *phase* ya mambo mazito kweli kweli na sasa *EAR* inaongezewa nguvu kufuatana na *experience* ya miaka mitano tuliyoiona. Kwa hiyo, tunaamini kwamba mtakuwa ni Maaskari ambao mtakuwa na Kasi na Nguvu

Mpya, na Ari Mpya. Kwa hiyo, mimi napenda kushukuru sana wale wote ambao wameni- *support* ni wote, hakuna mtu hata mmoja aliyesema hanipi kura, wote tumekuwa *busy* hapa hata hawa wenzangu ambao tumechuana hapa kwenye chumba cha kungojea pale tulikuwa ni furaha tupu na naamini ile furaha itaendelea maana tumefahamiana kwa namna ambayo hapo kabla tulikuwa hatufahamiani na wengine. Kwa hiyo, tunawatakiya kila heri na mimi nasema nawashukuru sana kwa kura ambazo mmenipa ambazo ni nyingi, pamoja na kwamba kwa mchuano ambao ulikuwepo hazikutosha kufuatana na nafasi zilizokuwepo, lakini nawashukuru sana, ahsante sana. (Makofi)

DR. NORMAN A. SIGALLA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme ninashukuru sana, tena sana kwa uchaguzi huu, jambo kuwa nimeweka rekodi nafikiri kuwa Mbunge kijana ambaye pia nimetumikia kwa muda mfupi labda kuliko Mbunge mwingine yoyote katika historia ya Tanzania ukiachia kufa na mambo mengine, kwa maana ile ya kuondolewa kwa kura halali.

Mheshimiwa Spika, nimesema ninashukuru sana kwa kura nilizopata, lakini na ninasema tena ya kwamba pamoja na ujana wangu, nadhani nimeweka historia kwa sababu ni Mbunge kijana niliyekaa muda mfupi zaidi nadhani kuliko Mbunge yoyote, toka tupate uhuru, kwa maana ya kuondolewa madarakani kwa kura, miezi saba iliyopita umewekwa kwa kura na Wabunge hao hao miezi saba baadaye wanasema hapana, nadhani ni historia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakubali kabisa kwamba sayansi ya Siasa haina kanuni, huwezi kusema moja jumlisha moja ni mbili. Jana wakati naongea na kaka yangu Prof. Wangwe nilimtania kidogo, akaniambia nadhani mambo yanaweza yakabaki vilevile, nikasema Mheshimiwa Profesa, *you may prove to be wrong* kwa sababu hawa wapiga kura wanabadilika kila dakika. Nadhani nilichokuwa nasema jana kimethibitishwa leo.

Mheshimiwa Spika, ninaipenda Serikali yangu ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyoniivisha na kuwa na sifa hizo ambazo ninazo, ninakipenda Chama cha Mapinduzi, ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyoniwezesha mimi kuiva hivi nilivyoiva kwa sababu hiyo ninaamini kabisa utumishi wa Dr. Norman Adamson Sigalla hauko kwenye Ubunge tu, maadam Serikali ndio hii hii ninafahamu kwamba Dr. Sigalla yupo bila shaka atakuwa na mahali pa kutumika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo niwashukuru ninyi nyote Wabunge wa kike kwa wakiume kwa kunitia moyo katika kipindi changu chote nilichokuwa Afrika Mashariki, nishukuru sana wenzangu ambao wako Afrika Mashariki sasa na hasa Mheshimiwa Abrahaman Kinana, kwa juhudi zote alizokuwa akizifanya kututia moyo na hata kujenga jina kwenye medani ya kimataifa hasa ukichukulia Afrika Mashariki. Tunazochangamoto chache, ni vizuri niziseme maadamu ni mahali sahihi pa kusemea, tunayo changamoto kubwa kwenye kupungua kwa maji kwa ziwa Victoria. Ninaombeni sana hao wanaochukua nafasi zetu wakumbuke wazi kabisa kwamba changamoto iliyonayo Tanzania ni kwamba sehemu kubwa ya maji yanayopungua ni kutokana na

chanzo kingine kilichojengwa Uganda kinachozalisha umeme. Kwa hiyo, huko kuna dana dana nyingi zinapigwa lakini ndiyo hali halisi. Lakini *damages* hathali tunazozipata ni Tanzania zaidi kwa sababu asilimia 49 ya ziwa lile liko upande wetu, baada ya kusema hayo nirudi tena kuwashukuru sana kwa upendo mlionipa katika kipindi chote ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, Dr. Sigalla endelea kujiimarisha, ni kijana safi, na hakika siku za usoni utafika mbali. Sasa kwa kundi hili naona pia tumemaliza kwa sababu simwoni Dr. Kasungu, labda sijui Mr. Mmanda, ahsante sana karibu.

ND. EVOD M. HERMAN: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo, tulikutoka ni mbali.

Pili, napenda nikishukuru Chama changu Chama cha Mapinduzi, nasema hivyo sio kama *fashion*, bali kwa kuweza kuniamini mpaka leo hii nimesimama hapa, ni hatua kubwa sana katika maisha yangu. Tulipokuja hapa ninaamini hatukuja kushindana, tulichujwa vizuri sana hasa tuliotoka Chama cha Mapinduzi, tulikuja kujipanga na katika kujipanga wamepatikana watakaotuwakilisha. Rai yangu ni kwamba, tuwaunge mkono kwa hali na mali kwa sababu kupunjika kwa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni hasara yetu sisi sote, sio hasara ya watu tisa.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi na Bunge lako kwa kutupa heshima ya kuingia ndani ya Bunge, hata kusimama kwenye mimbari za Mawaziri, kulihutubia Bunge kuomba kura na Waheshimiwa Wabunge wakatusikiliza na wakatupa kura. Naomba nishukuru kwa kuwa mimi ni mara ya kwanza na kwa uchanga nilionao ninaoufahamu nilichokipata sio kidogo, ni kikubwa sana. Nawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awasaidie, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, sasa kundi la Bara, kumbe ndio hili tumelimaliza, nilitaka kurudia tena. Sasa baada ya kumaliza utaratibu wa wale ambao tumewachagua Wabunge wateule wa Bunge la Afrika Mashariki, nikianza mwanzo ni Mheshimiwa Septuu Mohamed Nassor asimame, Mheshimiwa Janeth Deo Mmari, Mheshimiwa Kate Sylvia Kamba. Basi, nawaomba mmekeki.

Wanafuatiwa na kundi la Tanzania Zanzibar, Mheshimiwa Abdallah Ali Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, ahsante mkeki.

Kundi la Vyama vya Upinzani ni Mheshimiwa Fortunatus Lwanyantika Masha, sikutaka kusema mapema kwamba Dr. Masha nimesoma naye Tabora *School* kwa sababu ingekuwa ni kampeni, lakini naomba mfahamu hilo kwamba Spika na Dr. Masha tulikuwa pamoja Tabora *School*. Kwa nafasi hii, Dr. Masha nadhani tutaweza kuendelea kubadilisha uzoefu wa mambo mbalimbali, hongera sana. (*Makofi*)

Mwisho, Dr. Aman Walid Kabourou, bado sijakwambia ukae. Huyu naye alipoingia CHADEMA kwa sababu ni jirani yangu Urambo na Kigoma tunapakana,

nilimwomba ahamie Chama cha Mapinduzi miaka saba iliyopita, lakini Kigoma *Airport* pale akanitolea nje, akakataa. Nadhani uzoefu wa miaka saba ameona mwenyewe kwamba kwa kweli Chama ambacho kinapendwa na Watanzania ni CCM, karibu sana. Leo hii Dr. Kabourou unaonja matunda ya Chama cha Mapinduzi, ahsante sana. Dr. George Francis Nangale na kinara wao kwa kundi hili Dr. Didudas John Massaburi. *(Makofi/Vigelele)*

Sasa Waheshimiwa, kwa haraka haraka bila maneno mengi kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wamewasikilizeni siku nzima lakini ni utamaduni kwamba mtu unashukuru. Kwa hiyo, nikianza kwa kundi la wanawake, naomba sasa Mheshimiwa Mbunge mteule wa EALA, Sebtuu Mohamed Nassor, uweze kuja. Sasa itabidi uje hapa maana yake Mbunge uje hapa sasa, leo ni siku ya kuweza kujitambulisha vizuri, Katibu angalia *microphone* hiyo.

MHE. SEPTUU MOHAMED NASSOR: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, awali ya yote kwanza natoa pongezi zangu kwako wewe pamoja na Bunge kuweza kufanikisha uchaguzi huu. Mchakato huu ni wa muda mrefu, lakini leo umefikia mwisho na naomba kusema umesema tusichukue muda mrefu, naomba kuongeza tu, naelewa kwamba tumewachosha sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuwafuatafuata, kwa kuwapa makaratasi, lakini ndio utaratibu wenyewe unavyokuwa. Kwa hiyo, naomba mtusamehe.

La pili, naomba kwa nafasi hii niliyopewa hapa kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kunifikisha hapa hii leo nikaweza kusimama mbele ya Bunge hili na kwa heshima uliyonipa kuja kuhutubia hapa, ahsante sana. Tena nawaomba Wabunge wale ambao wamenipa kura na wale ambao hawakunipa kura wawe na imani na mimi kabisa kwamba nitaiwakilisha Tanzania na watu wake katika shughuli zote zinazotakiwa na vilevile nitaitetea Tanzania pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

MHE. JANETH DEO MMARI: *Honourable Speaker, Honourable Member's of Parliament, Ladies and Gentlemen, I wish to take this opportunity to thank every person who participated in this process right from the beginning, let say from particle class up to the Parliament.*

Honourable Speaker, I believe the East Africa Community is for the East African's and thirty million plus Tanzanian's for this reasons I believe that an MP, representing Tanzania, I represent each Tanzania who are represented by all the people sitting around here. (Applause)

I certainly feel heavily invented for the trust that of given to me and for that reason, I am prepared to work and please anybody who feel that she or he has anything that I can do, that will help, the every Tanzanian who is in the village because the East African Community is for the Tanzanian's not for the secretariat, not for the summit, not

for the Minister or for anybody working for the community let that person contact me so that we can work together.

Honourable Speaker, I may stand to be corrected but I believe there is no an excess between this Parliament and East African Community Parliament. However, I take note that there is full fleshed Ministry of East African Affairs and I believe this Parliament and Ministry will work together so that there can be established an excess so that the people you have elected today, can take the challenge that responsibility of working for Tanzanian, whom you present and you have appointed us, with those few remarks let me say thank you and I can't thank you enough. (Applause)

SPEAKER: *Thank you Mrs. Mmari, now will hear from Kate Sylvia Kamba.*

MHE. KATE SYLVIA KAMBA: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, nimesimama hapa kwa unyenyekevu mkubwa kabisa, kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha salama katika saa hii na kwa kura zenu nyingi ambazo mmenipatia kuniwezesha kurudi tena kwenye Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Ninawashukuru sana kwa heshima ambayo mmetupatia, tulikuwa tisa, katika Bunge lililopita na katika hao tisa waliorudi ni wawili, tutajitahidi kuendeleza ile *institution memory* ya *East African Community* ambayo ipo kati yetu wawili ambao tumerudisha na tunaahidi kwamba tutaendelea kufanya kazi kwa bidii zote, tukishirikiana na Kamati ya mambo ya nchi za nje ndani ya Bunge letu, katika kuimarisha yale yote mtakuwa mnatutuma.

Tunaamini kwa ushirikiano wa pamoja Wabunge waliochaguliwa na sisi sote ndani ya Bunge hili, tutaisukuma *East Africa*, nawashukuruni sana sana, Mungu aendelee kuwabariki na Mungu aendelee kuibariki nchi yetu, tuendelee kukaa kwa upendo na amani na wale ambao wamekosa wasikate tamaa. Nafasi zilikuwa chache na watu ni wazuri mno, lakini wamechaguliwa wachache ndio sisi ambao tunakwenda kuwawakilisha. Kidumu Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

SPIKA: Huo ndio mwisho wa kundi A, kundi B tutaanza na Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal.

MHE. DR. SAID GHARIB BILAL: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, awali ya yote na mimi naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuweko hapa wakati huu.

Pili, naomba nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunitua mimi kuanzia Kamati maalum Zanzibar hadi Kamati Kuu na kwisha *authority* yake kwa Kamati ya Bunge na hatimaye kuweza kuchaguliwa hapa mimi leo. Nasema kwamba wakati wote huo, imani ya Chama cha Mapinduzi ilianza tangu Kamati Maalum, nawashukuru kwamba Wabunge wameendeleza imani iliyonipa Chama changu hadi kufikia kuchaguliwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuchukua fursa kushukuru familia yangu hasa kwa kuni-*encourage* kuingia katika mashindano haya kwa kuamini kwamba Chama cha Mapinduzi kinafanya demokrasia katika awamu zote, nashukuru sana kwa kunipa *support* familia, ahsante.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wangu mimi wa Bunge la Afrika Mashariki ni kwamba, sisi ni *extension* ya Bunge lako Tukufu na kwa kupitia Bunge lako Tukufu ni *extension* ya wananchi. Kwamba Afrika Mashariki mambo yote yanayokuwa yanapitishwa pale yanahitaji kuangalia wadau wote wakiwemo Serikali *Business Community* na wananchi wa Tanzania na nataka nikuhakikishie kwamba tunaelewa kwamba Afrika Mashariki inawakilisha dhamira na niseme ndoto, lakini ndoto za kweli za kuhakikisha kwamba Afrika Mashariki hatimaye itakamilisha matumaini ya eneo la Afrika Mashariki lenye watu zaidi ya milioni 100 kuwafikia katika maisha mazuri na hali bora ya kimaisha, nataka niahidi kwamba tutafanya kazi kama nilivyolelewa kama ni mtu wa utafiti wa *consultation* na mtu wa kusoma, nihakikishe kwamba haya yote tutayatumia katika kuhakikisha kwamba tunafanya nzuri kuwakilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru sana na nishukuru Bunge lako kwa kutuchagua na kutuamini na naahidi kwamba tutafanya kazi nzuri, ahsanteni.

MHE. ABDULLAH ALI HASSAN MWINYI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa ningependa kutoa shukrani za dhati kwa heshima kubwa mliyoniwa kijana wenu kwa kunipa kura nyingi za kishindo kabisa kuniwezesha kunifikisha katika Bunge la Afrika Mashariki. Napenda kusema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Sina mengi ya kusema na malipo yangu kwenu ni jitihada kubwa ambayo nitaifanya katika Afrika Mashariki, kutetea maslahi ya Taifa letu, ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Kundi C, napenda nimwite rafiki yangu Dr. Masha aweze kutuhutubia.

MHE. DR. FORTUNATUS L. MASHA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wote, labda nitumie msembo ambao nimeusikia mahala, mimi nilikuwa mgombea mwaka 2001, kura hazikutosha, leo zimetosha sana. (*Makofi*)

Kwa kuwa ni nafasi ya kutoa shukrani nianzie ambako nimeanzia, kama sio Chama changu cha *UDP* kunitewa hata nisingefika hapa kura zikatosha. Kwa hiyo, nataka kutoa shukrani kwa Chama changu cha *UDP* kwa kunitewa na kunifikisha hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba kuna Mbunge mmoja wa *UDP* katika Bunge hili, rafiki yangu na Mwenyekiti, wangu Bwana Mapesa, kwa hiyo, haikuwezekana kwamba nimepata kura yake ikazaa mpaka zikawa 202, nataka kutoa shukrani kwenu nyote mlioniamini na kunipa kura nyingi namna hiyo. Nafahamu wana-

CCM wengine walitoka, kwa hiyo, hizo kura nyingi ni za wana-CCM, nataka kuwashukuruni sana. *(Makofi)*

Nakuwahakikishieni kwamba tutafanya kazi kwa pamoja na kwenda Bunge hili la Afrika Mashariki sio kama mjumbe wa *UDP* hapana, sio kama mjumbe wa upinzani hapana, mimi wenzangu tunakwenda kama Watanzania. Nataka kuwaahidi wenzangu wanaotoka Chama cha CCM wasiwe na wasiwasi na mimi katika ushirikiano wetu tukiwa pamoja.

Nataka kumhakikishia Waziri wa Mambo ya Afrika Mashariki na wengine wote ambao watakuwa na ujumbe wa kutupa wasisite kunifikia kwa sababu mimi natoka kundi la upinzani lakini mimi ni Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kushukuru kwa maneno uliyoanza nayo ulipotaja jina langu leo mchana na mimi hapa moyoni najisikia hivyo hivyo kwa kumbukumbu zetu za *Tabora School*. Kuna wengi ambao wamenisaidia kufika hapa, wapo wengi mno nikiwataja itachukua muda mrefu sana, lakini nataka wote wafahamu kwamba ninawashukuru sana. Labda tukitoka nje, nitapata nafasi ya kuwapa shukrani moja kwa moja lakini kwa ujumla wenu nasema ahsateni sana na Mungu aibariki Tanzania. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Dr. Masha, lakini kwa taarifa tu ya hawa ambao ni wachanga kidogo katika siasa ni kwamba Dr. Masha alipata kuwa Katibu Mwenezi wa *TANU*. *(Makofi)*

Tunaendelea sasa. Lakini sasa Mheshimiwa Kingunge anisamehe kidogo labda niseme kundi la Vingunge. Nitaanza na jirani yangu Dr. Aman Walid Kabourou.

MHE. DR. AMAN WALID KABOUROU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Sana Wabunge wote na mimi kwanza nianze tu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama changu cha Mapinduzi ambacho nimenifikisha hapa. Sisemi hivyo kama alivyosema Ndugu yangu labda kwa fasheni lakini ni kwa ukweli kabisa.

Mheshimiwa Spika, amesema neno zito kwamba alijaribu kunishawishi niingie CCM miaka saba iliyopita na mimi nikagoma nikajaribu kuvumilia katika vyama vya upinzani na nikagundua kwamba havitakiwi na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kusema kwamba usione aibu na wala hukuwa peke yako katika kufanya hivyo kuna wengi siwataji hapa walionishawishi nifanye hivyo na mimi nikawa nimegoma. Lakini wamasema katika vitabu kwamba;

“Mchungaji Mwema ni yule anayewaacha Kondoo wake 99 akamfuata yule mmoja aliyepotea“

Huyu ndiye mchungaji mwema na ninasema Chama Cha Mapinduzi ni Mchungaji Mwema kwa sababu wameweza kuwaacha hawa Kondoo 99 wakasema yule anapotea mrudisheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kondoo yule amerudi na mimi nasema kwa uhakika kabisa kwamba naitakitetea Chama changu na ninao uwezo wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, mimi nishukuru tu kwa jinsi uchaguzi wetu ulivyokwenda na kwa jinsi ambavyo matokeo yetu meonyesha ah! kumbe yale maneno ya mizengwe sio kweli katika Serikali inayoongozwa na CCM mara zote chaguzi zote zinaendeshwa kiuwazi na kiuhalali kabisa na hata mimi nimeweza kujionea kwa macho yangu. Sikupeleka hata wakala katika kuhesabu mambo ya kura.

Napenda niwashukuru Ndugu zangu Wabunge kwa heshima kubwa mliyonyesha na mimi naahidi kabisa kwamba huko *East Africa* nitafanya kazi nzuri nikishirikiana na Ndugu zangu tuliochaguliwa pamoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Aman Walid Kabourou lakini ombi la Spika ni kwamba kwa faida ya nchi wewe na mwenzio Mbunge wa Kigoma Mjini Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba mtafanya kazi kwa pamoja, Kigoma inawahitaji nyote wawili mshirikiane. *(Makofi)*

Sasa namuita Dr. George Francis Nangale.

MHE. DR. GEORGE FRANCIS NANGALE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge, awali ya yote ningependa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Chama changu cha Mapinduzi kwa kuiteua kwa mara nyingine kusimama katika nafasi hii kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wabunge wote na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyingine kulitumikia Taifa letu katika nafasi ya Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Napenda niwaahidi kwamba nitashirikiana na wenzangu na kwa sababu nimeshapata uzoefu wa miaka mitano ya mwanzo nitashirikiana na wale wapya kuimarisha *Tanzania Chapter* ili iwe *effective* zaidi na kusimamia maslahi ya nchi yetu katika siku zijazo kwa sababu suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki siyo suala la hadithi ni suala la halisi *it is reality* na kwamba hatuna *option* isipokuwa kwenda huko.

Kwa hiyo, tunachohitaji kufanya ni kuhakikisha kwamba Wawakilishi wetu wanawakilisha maslahi ya nchi yetu na tuwe viongozi katika kusimamia hii *process* ya *intergration* tusiwaachie wenzetu ndiyo watusimamie, ni ukweli kwamba Tanzania ndiyo nchi yenye raslimali kwa wingi katika eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri basi tukatumia uwezo huo tulionao *including* raslimali ya watu wenyewe yaani *Human Resource* kuhakikisha kwamba tuna – *play a leading role* katika *intergration process* yetu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mwisho kabisa ningependa kuwaahidi kwamba tutaendelea kwa 100% *commitment* na kama usemi wako unavyosema *with Speed and Standards*. (Makofi)

Ahsanteni sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Nangale tunahitimisha sasa kwa Mbunge Mteule Dr. Didas John Massaburi. (Makofi)

MHE. DR. DIDAS JOHN MASSABURI: Mheshimiwa Spika, nami kama wenzangu waliotangulia napenda kwanza nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi na hasa Kamati Kuu ya Chama ambayo ilikubali kuteua jina langu ili liweze kupitishwa na Kamati ya Wabunge wa CCM kugombea nafasi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, naomba niwashukuru Wabunge wote kwa ujumla wao kwa jinsi ambayo wamenipa kura za kutosha safari hii kwa sababu mara ya kwanza hazikutosha kule kwenye Kamati ya Wabunge wa CCM, kwa hiyo, niwashukuru kwa dhati kabisa na niwaombe waelewe kwamba mimi nitakachokifanya kule Afrika Mashariki ni kwenda kuwatumikia Wabunge wa Bunge hili pamoja na wananchi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nimshukuru kwa dhati kabisa mke wangu Janeth Mourice Massaburi kwanza kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuniliwaza wakati wote nilipokuwa na majonzi, ilikuwa nikipata dhoruba kali kwenye kampeni wengi wenu mlikuwa hamwoni machozi yangu, lakini yeye alikuwa akiyafuta. (Makofi)

Nne, niwashukuru Wakubwa wangu wa Kazi, Waziri wangu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Manaibu Waziri Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila na Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza kwa kuniruhusu kwanza na ninawashukuru kwa majonzi kwa maana kwamba huenda nitaacha kufanya kazi katika Wizara ile lakini nadhani nitakuwa nao daima katika utendaji wowote watakapohitaji kunitumia mimi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba mimi ni Mtumishi wenu kwa hiyo msisite kunituma na ninaahidi kwamba sitawaangusha. Ahsanteni sana. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimepata maombi mengi sana ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanataka kuzungumza, lakini ninasikitika sitaweza kuyaruhusu. Kwanza haipendezi wenzetu pamoja na kwamba wanasema sisi tumechoka lakini nadhani wao wamechoka zaidi. Kwa hiyo, kibinadamu inafaa tuwape nafasi ya mapema wavishwe mashada ya maua, wazungumze na wenzako, wale wenye fursa ya faraja kama alivyo Mheshimiwa Dr. Massaburi tukiendelea humu na Mheshimiwa Janet Massaburi ni Mbunge mwenye nidhamu akiendelea kukaa humu tu mambo yanakwenda kule Mume wake keshatoka haiwezi kupendeza. Kwa maana hiyo na kwa heshima

kubwa na taadhima tunaye msemaji ambaye anaweza kwa ufasaha kabisa na kwa uhalali akaweza kuwatuma Wabunge wateule hawa tisa wa Tanzania wajue huko wanakokwenda kwamba wana baraka zetu na awape ujumbe wa nini tunategemea sisi tu Wabunge lakini na wananchi waliotuchagua.

Namwita Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa ili aweze kusema kidogo.
(*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, yuko kiongozi mwenzetu wa Chama cha Mapinduzi lakini ni Marehemu sasa nadhani hapa angependa kusema lugha hii: “Haijapata Kutokea!” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya pekee kabisa niweze kusema machache ya kuwapongeza wenzetu waliochaguliwa kuingia Bunge la Afrika Mashariki. Lakini kabla ya kufanya hivyo, nina hakika nitasema kwa niaba ya Wabunge kwamba tunakupongeza wewe na Ofisi yako kwa kazi nzuri sana ya kuandaa uchaguzi huu, mmefanya kazi nzuri ya uwazi kabisa na mmeona wenyewe hata wagombea kila mmoja aliyesimama ameshukuru na ameridhika kwa mambo yalivyokwenda. Tunawapongeza kwa kazi nzuri sana pamoja na Sekretarieti yako.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi leo nimesononeka sana kwa kitendo kilichotokea kwa wenzetu wa upinzani kutoka nje ya Ukumbi wa Bunge, lakini kanikumbusha kila siku tukizungumza na Viongozi wenzetu wa Zanzibar huwa wanatuambia: “Kwani ninyi hamuwajui *CUF*?” Leo nakiri wenzetu wa Zanzibar kweli wako sawasawa hatuwajui *CUF*, maana jambo la demokrasia kama hili limepata mjadala, hata kabla mjadala haujakwisha, watu kwa hasira wametoka nje ya Ukumbi wa Mkutano kabda uchaguzi haujafanyika tena watu wenyewe ni watu wasomi. Kwa kweli ni kitendo cha aibu sana! Najipa faraja moja tu kwamba sasa Watanzania wanapata nafasi ya kuwafahamu *CUF* ni nani na ndiyo wanahalalisha kauli aliyotoa Mheshimiwa Kabourou muda mfupi uliopita kwamba hawakubaliki kwa wananchi. Sasa wasitumie mbinu za hovyoko kutaka kukubalika. Lakini niruhusu nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wale Wabunge wa Upinzani waliokuwa makini, waliokomaa na wakabaki ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa madhumuni ya *Hansard* nataka kuweka shukrani zetu na pongezi zetu kwa kuonyesha ukomavu wa kisiasa. (*Makofi*)

Wabunge hao wa Upinzani ni pamoja na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya na Mheshimiwa John Momose Cheyo. Tunawapongeza sana. Ninyi mmeonyesha ukomavu wa kisiasa sasa waambieni hao marafiki zenu wajifunze kutoka kwenu wasitutie aibu katika nchi yetu. Mimi ningependa kwa heshima ambayo Bunge letu limejenga, kwa demokrasia ambayo inaonekana ndani ya Bunge letu kitendo cha leo kimetudhalilisha na kutupa aibu. Nakubaliana na pendekezo lako kwamba Kamati moja itafakari hawa jamaa wachukuliwe hatua gani za kinidhamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwa Waheshimiwa Wagombea. Mtakubaliana nami kwamba siku hizi tulizokaa hapa Dodoma zimekuwa changamoto kwelikweli. Sina nafasi ya kupita sana Mtaani, lakini kila saa nilikuwa napigiwa simu nikiambiwa: “Mzee mambo yamebadilika!” Ilikuwa kama *temperature* za Malaria zinapanda na kushuka kila mara. Mara unasikia Samwel Mwitwa Wangwe kaongoza, mara unasikia Dr. Didas John Massaburi, lakini ah! Nawapongeza sana, mmefanya kazi ya kutukomaza vizuri sana. Kila mmoja amefanya kampeni yake kwa umakini na umahiri wa hali ya juu sana. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Kwa wale ambao hamkuchaguliwa, nakubaliana na lugha aliyotumia Mzee Masha kwamba kura hazikutosha. Sio kwamba ninyi hamkutosha, bali kura tu hazikutosha na *inshallah* siku moja zitatoshia. Lakini nakubaliana pia na Mheshimiwa Sigalla kwamba sasa mmeonekana kwamba ni wanasiasa. Nafasi hizi ziko nyingi, siyo Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini zipo nyingi na nyinginezo kuna nafasi ya kuonekana. (*Makofi*)

Nawapongeza vilevile kwa kukubali matokeo ya uchaguzi, nawapongeza sana. Kwa wale waliochaguliwa nawapongeza na hongera sana mnastahili. Lakini mnakwenda kwenye Bunge la Afrika Mashariki si kama *UDP* na Chama Cha Mapinduzi, mnakwenda kama Wawakilishi wa Serikali na Watu wa Tanzania. Tumeelezwa toka kampeni zilipoanza kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ina changamoto za kisasa na kubwa sana. Tumewachagua kwa niaba ya Watanzania kwa kuwaamini kwamba mtatuongoza vizuri katika changamoto hizo maana mnaweza kutuongoza vizuri. Lakini muende kama timu moja ya mpira na timu hiyo ifunge goli. Najua ni katika mazungumzo, lakini mazungumzo ni *give and take*, lakini yule mjanja hupata mengi zaidi na ninyi kuweni wajanja, Watanzania wapate mengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuwapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. Wale wa Chama Cha Mapinduzi wanajua mashaka yaliyokuwepo lakini mashaka yote yale yametoweka. Si ndiyo Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru?! Mashaka yote yametoweka, hakukuwepo na udini, ukanda, ukabila lakini watu wamechaguliwa kutokana na uwezo na kila mmoja alivyofanya kampeni yake. Nawapongeza kwa sababu tunatoa sura sahihi na ujumbe sahihi kwa Watanzania kwamba Bunge letu ni Bunge imara lenye umoja, mshikamano na linaloangalia uwezo wa mtu na siyo atokako, kabila lake, dini yake wala kitu chochote. Nawapongeza sana kwa jambo hili mlilolifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua watu wamechoka, lakini nimesimama kwa niaba yenu kuwapongeza waliochaguliwa, waliojitokeza na kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa maandalizi mazuri sana na kuwapongeza wale wenzetu walioonyesha ukomavu wa kisiasa wa kubaki humu ndani na wale ambao wametoka wajue hawatuaibishi sisi kama Wabunge, bali wanajiaibisha wao kama Chama chao ambacho hakiwezi kushiriki katika malumbano ya kisiasa na kufikia muafaka bila kukimbia. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, baada ya salamu hizo nzito za Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali humu Bungeni Waziri Mkuu wetu sasa natamka kwamba

naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. Kuna rekebisho kidogo itabidi Waheshimiwa Wagombea na wale ambao wamepita, basi mtoke kwanza, lakini Waheshimiwa Wabunge tukae.

*(Saa 12:20 mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku yaJumaa,
Tarehe 03 Novemba, 2006 Saa 03:00 Asubuhi)*